# MIELEKEO YA WAUZA MIFUGO MNADANI WANAOZUNGUMZA KINANDI  KUHUSU KISWAHILIKATIKA KAUNTI  YA NANDI

**NA**

**ANNE JEPKEMBOI**

**C50/KER/CE/28396/2015**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**NOVEMBA, 2025**

# UNGAMO

Tasnifu hii ya Uzamili ni utafiti wangu binafsi na haijapata kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kingine.

JINA: ANNE JEPKEMBOI

(C50/KER/CE/28396/2015)

SAHIHI.............................. TAREHE 21·11·25

Tasnifu hii ya Uzamili imewasilishwa kwa idhini yangu kama msimamizi niliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

JINA: DKT. JACKTONE ONYANGO

SAHIHI.............................. TAREHE 21·11·2025

# TABARUKU

Ninatabaruku kwa wazazi wangu wapendwa Bw. Eliud Saina na Perpetua Saina pamoja na bamkwe mpendwa marehemu Samwel Letting na mamkwe Bi. Rosa Letting walionitia hamasa masomoni.

## SHUKRANI

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunibariki na afya njema muda wote wa masomo yangu.

Shukrani maalum kwa msimamizi wangu, Dkt. Jacktone Onyango, kwa kunielekeza ipasavyo kutoka hatua ya mwanzo hadi mwisho.

Ninamshukuru kwa dhati mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili, Prof. Peter Githinji na watahini walioisoma tasnifu yangu kwa umakinifu mkubwa na kunielekeza. Siwezi kumsahau mhazili wa Idara ya Kiswahili, Bi. Lucy Gachanja, kwa kufuatilia kazi yangu na kuhakikisha kwamba kila kitu kiko sawa.

Mwisho, ninawashukuru wote waliochangia kwa njia mbalimbali kunipatia usaidizi wa kila aina wakati nilikuwa nikifanya utafiti na kutayarisha tasnifu hii. Mungu awabariki nyote.

**YALIYOMO**

**UNGAMO ... ii**

**TABARUKU... iii**

**SHUKRANI... iv**

**YALIYOMO... v**

**ORODHA YA MAJEDWALI ... ix**

**ORODHA YA VIELELEZO... ix**

**ORODHA YA AKRONIMU NA VIFUPISHO... x**

**UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU... x**

**IKISIRI... xi**

**ABSTRACT...xii**

**SURA YA KWANZA... 1**

**UTANGULIZI... 1**

1.0 Dibaji... 1

1.1 Usuli wa mada... 1

1.2 Suala la utafiti... 4

1.3 Malengo ya utafiti... 4

1.4 Maswali ya utafiti...5

1.5 Sababu za kuchagua mada... 5

1.6 Upeo na mipaka... 6

1.7 Hitimisho...7

**SURA YA PILI...8**

**MAPITIO YA MAANDISHI NA NADHARIA ...8**

2.1 Utangulizi...8

2.2. Yaliyoandikwa kuhusu mada...8

2.2.1 Dhana ya mielekeo...8

2.2.2 Mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili............................................................ 9
2.2.3 Maendeleo ya lugha ya Kiswahili................................................................12
2.2.4 Historia ya mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya.......................................17
2.2.4.1 Mielekeo ya lugha katika kipindi cha ukoloni.......................................... 17
2.2.4.2 Mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya baada ya ukoloni...........................24
2.3 Misingi ya nadharia ya utendaji razini........................................................... 34
2.3.1 Mielekeo ya mhusika.................................................................................... 37
2.3.2 Utambuzi wa mhusika.................................................................................. 38
2.3.3 Tathmini ya mielekeo.................................................................................... 39
2.3.4 Tabia elekezi.................................................................................................. 39
2.3.5 Uthabiti wa vijenzi vya mielekeo.................................................................40
2.3.6 Kanuninafsi.................................................................................................... 40
2.4 Hitimisho.........................................................................................................41
**SURA YA TATU.........................................................................................42**
**MBINU ZA UTAFITI..................................................................................... 42**
3.1 Utangulizi.........................................................................................................42
3.2 Mbinu za Utafiti............................................................................................... 43
3.2.1 Muundo wa utafiti.......................................................................................... 43
3.2.2 Mahali pa utafiti.............................................................................................. 44
3.2.3 Kikundilengwa................................................................................................ 45
3.2.4 Uteuzi wa sampuli........................................................................................... 45
3.2.5 Utafiti wa awali................................................................................................ 46
3.2.6 Mbinu za ukusanyaji data............................................................................. 47
3.2.7 Uchanganuzi wa data..................................................................................... 49
3.2.8 Uwasilishaji wa data....................................................................................... 49
3.3 Maadili ya utafiti.............................................................................................. 50

3.4 Hitimisho ........................................................................................51

**SURA YA NNE.......................................................................................52**

**UWASILISHAJI WA MATOKEO NA MJADALA KUHUSU MIELEKEO YA WAUZA MIFUGO.......................................................................... 52**

4.1 Utangulizi........................................................................................ 52

4.2 Uwasilishaji wa matokeo.........................................................................52

4.2.1 Wasailiwa katika utafiti.................................................................. 53

4.2.2 Uchanganuzi wa mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu lugha ya Kiswahili.................................................................................54

4.2.2.1 Matumizi ya lugha na mielekeo kuhusu Kiswahili...................................57

4.2.2.2 Umri wa wauza mifugo na mielekeo kuhusu Kiswahili...........................58

4.2.2.3 Viwango vya elimu na mielekeo kuhusu Kiswahili.................................59

4.2.2.4 Jinsia na mielekeo kuhusu Kiswahili.......................................................61

4.3 Mjadala kuhusu uchanganuzi wa mielekeo ya wauza mifugo.........................61

4.3.1 Mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi........................................................................................ 62

4.3.2 Vipengele vinavyosababisha mielekeo mbalimbali ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili..........................................................................65

4.3.2.1 Umri wa wasailiwa.........................................................................65

4.3.2.2 Uhusiano uliopo kati ya umri na kuchanganya lugha................................70

4.3.2.3 Viwango vya elimu........................................................................74

4.3.2.4 Jinsia........................................................................................78

4.3.3 Athari za mielekeo ya lugha kwa maendeleo ya Kiswahili katika jamii.......82

4.4 Hitimisho........................................................................................87

**SURA YA TANO.......................................................................................89**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO......................................89**

5.1 Utangulizi........................................................................................89

5.2 Muhtasari wa utafiti..........................................................................89

5.3 Matokeo ya utafiti........................................................................................91
5.3.1 Mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi....................................................................91
5.3.2 Mambo ambayo husababisha mielekeo tofautitofauti kuhusu lugha ya Kiswahili miongoni mwa wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi..............................................................................................................92
5.3.3 Mielekeo ya lugha na athari zake kwa maendeleo ya Kiswahili..................93
5.4 Changamoto za utafiti......................................................................................94
5.5 Mapendekezo ya utafiti zaidi...........................................................................96
5.6 Hitimisho..........................................................................................................98
**Marejeleo**.......................................................................................................100
**VIAMBATISHO......................................................................................109**
Kiambatisho 1: Barua ya kujitambulisha kwa wasailiwa...................................109
Kiambatisho 2: Hojaji kwa wauza mifugo mnadani............................................110
Kiambatisho 3: Maswali ya viwango kwa wauza mifugo mnadani.....................113
Kiambatisho 4: Bajeti ya pendekezo..................................................................115
Kiambatisho 5: Kibali cha utafiti........................................................................116
Kiambatisho 6: Ramani ya Kaunti ya Nandi.......................................................118

## ORODHA YA MAJEDWALI

3.1 Uteuzi wa sampuli..........................................................................................46

4.1 Majibu ya maswali ya viwango vya mielekeo kwa wauza mifugo mnadani.....................................................................................................56

4.2 Matumizi ya lugha na mielekeo kuhusu Kiswahili ........................................58

4.3 Umri wa wasailiwa katika utafiti....................................................................58

4.4 Viwango vya elimu.........................................................................................60

4.5 Jinsia...............................................................................................................61

4.6 Mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi...........................................................................................63

4.7 Viwango vya elimu vya wasailiwa................................................................76

4.8 Matokeo ya mielekeo kijinsia.........................................................................79

4.4 Athari za mielekeo ya lugha kwa maendeleo ya Kiswahili katika jamii...................................................................................................84

## ORODHA YA VIELELEZO

2.1 Mielekeo na utabiri wa tabia..........................................................................35

4.1 Mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi...........................................................................................64

4.2 Umri wa wasailiwa katika utafiti................................................................... 66

4.3 Viwango vya elimu vya wasailiwa................................................................77

4.4 Matokeo ya mielekeo kijinsia.........................................................................79

## ORODHA YA AKRONIMU NA VIFUPISHO

**BBC** - British Broadcasting Corporation

**COVID-19** - Corona Virus Disease

**NACOSTI** - National Commission for Science, Technology and Innovation (Kamisheni ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu)

**SPSS** - Statistical Package for Social Sciences (Programu ya Uchanganuzi wa data za Kitakwimu za Sayansi Jamii)

**TPB** - Theory of Planned Behaviour (Nadharia ya Tabia Ratibiwa)

**VoA** - Voice of America

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

**Wauza mifugo mnadani:** Ni watu waliokomaa na wanaoshiriki biashara ya kunadi mifugo.

**Wingi lugha:** Hali ya kutumia lugha mbili au zaidi na mtu mmoja au jamii.

**Mielekeo:** Hisia wanazokuwa nazo binadamu kuhusu lugha yao au ya watu wengine.

**Umilisi:** Uwezo wa mtu kutumia kanuni za lugha fulani.

**Sera ya lugha:** Mipango ya serikali kuhusu utumiaji wa lugha.

**Lugha ya taifa:** Lugha inayotumika kwenye shughuli zote za kitaifa na kuwaunganisha kimawasiliano watu wanaotoka katika jamii mbalimbali nchini.

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kueleza jinsi mielekeo ya wauza mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi kuhusu lugha ya Kiswahili inavyoathiri matumizi yao ya lugha. Mwelekeo wa watu kuhusu vitu au dhana unaweza kuathiri wale watu au dhana hizo. Tafiti tofauti zilizofanywa kuhusu mielekeo ya watu kwa lugha zimebaini kuwa mielekeo ya watu huweza kuwa hasi au chanya kutegemea masiala mbalimbali kama vile elimu, umri, mazingira, jinsia na kadhalika. Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo: kupambanua mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kwa lugha ya Kiswahili katika kaunti ya Nandi; kubainisha mambo ambayo husababisha mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu lugha ya Kiswahili na kuchunguza athari ya mielekeo hiyo ya lugha kwa maendeleo ya Kiswahili katika jamii hii. Nadharia ya Utendaji Razini (Theory of Reasoned Action) iliyoasisiwa na Fishbein na Ajzen (1975) ilitumiwa kuongoza utafiti huu. Wataalamu hawa wanasema kuwa binadamu ni viumbe wanaofikiria na wanajua aina ya mielekeo na tabia walizo nazo. Kwa hivyo, maelezo ya watafiti hawa yanalingana na lengo la utafiti huu ambalo ni kueleza matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wauza mifugo mnadani ambao mielekeo yao hudhihirika kupitia matumizi yao ya lugha. Utafiti huu ulihusisha wauza mifugo 35 kutoka minada yote 7 katika kaunti ya Nandi. Mtafiti alitumia idadi hii kimaksudi. Utafiti huu ulitumia mbinu ya utafiti wa maelezo ambapo data ilikusanywa kupitia hojaji, mahojiano na kushiriki utendaji kisha ikachanganuliwa na kuwasilishwa kupitia majedwali, baa grafu na pai chati. Ilibainika kwamba wauza mifugo mnadani wana mitazamo hasi kuhusu utumiaji wa Kiswahili kwa sababu wanahisi Kiswahili ni kigumu kwao. Matokeo ya utafiti huu yanaweza kutumiwa na washikadau mbalimbali wanaohusika na lugha ili kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa Wakenya wote wanafahamu na kutumia kwa ufasaha lugha ya Kiswahili ili wabadili mielekeo yao hasi kuhusu lugha hii.

## ABSTRACT

This study sought to investigate the use of Kiswahili language amongst livestock sellers in Nandi County especially how their attitude affects language use. The attitude of the people towards objects or concepts may affect those people or concepts. Different studies about people's attitudes have shown that their attitude may be positive or negative depending on factors like education, age, environment, gender among other factors. This research was guided by the following objectives: to identify different attitudes on the use of Kiswahili language among Nandi speakers who are livestock sellers in Nandi County; to determine factors that may cause different attitudes on Kiswahili language use among Nandi language speaking livestock sellers in Nandi County; and to find out the effects of such attitudes on the development of Kiswahili language in the community. This research was guided by the Theory of Reasoned Action (TRA) developed by Fishbein and Ajzen (1975). These scholars believe that there is a relationship between attitude and behavior. They say that people are creations who reason and understand the kind of attitudes and behaviour they have. Therefore, it is in line with the objective of this research which is to establish use of Kiswahili among livestock sellers whose attitude is portrayed through their use of language. 35 livestock sellers were purposively sampled from all the 7 livestock auctions in Nandi County. This study utilized descriptive research design where self administered questionnaires, interviews and participation were used to collect data for this study. The data was analyzed descriptively by use of mixed methods and information presented using bar graphs, frequency tables and pie charts. It was found out that those livestock sellers auctioning livestock at the market have negative attitude towards the use of Kiswahili language because they find it difficult. The research findings may be used by the concerned stakeholders to lay strategies to ensure that all Kenyans understand and use Kiswahili language correctly so that they can correct their attitude towards this language.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Dibaji

Sura hii inatoa maelezo kuhusu vipengele vya kimsingi katika utafiti huu ambavyo ni: usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, na upeo na mipaka ya utafiti.

## 1.1 Usuli wa Mada

Utafiti huu ulilenga kueleza matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi katika kaunti ya Nandi hasa jinsi mielekeo inavyoathiri matumizi yao ya lugha. Vilevile ulilenga kubainisha mambo ambayo husababisha mielekeo hiyo ya lugha miongoni mwa wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi na athari za mielekeo hiyo kwa maendeleo ya Kiswahili katika jamii.

Kimsingi mielekeo inaweza kuelezwa kama hisia ambazo watu huwa nazo kuhusu lugha wanayotumia au lugha inayotumiwa na watu wengine au vitu fulani (Fasold, 1984). Kulingana na Smith (1996), mielekeo ya watu kuhusu lugha aghalabu ni hisia hasi au chanya wanazozidhihirisha wajipatapo kwenye hali zinazowataka kufanya uamuzi kati ya lugha na hali mbalimbali za matumizi ya lugha. Binadamu wanaweza kuwa na mitazamo fulani kuhusu lugha yao au lugha ya wengine au zote kwa pamoja. Mitazamo ya jamii kuhusu lugha fulani ni moja kati ya mambo

yanayoweza kuathiri kwa njia hasi au chanya ukubalifu wa lugha iliyopendekezwa. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu lugha ya Kiswahili kupitia matumizi yao ya lugha hii katika shughuli zao mnadani.

Triandis (1971) anaeleza mielekeo ya lugha kama hali ya kuienzi au kutoienzi lugha fulani kwenye mazingira ya wingi-lugha. Naye Muthwii (2002) anasema kuwa wenyeji wa lugha huwa na mielekeo chanya kuhusu matumizi ya lugha ya mama hasa katika sehemu za mashambani. Katika kaunti ya Nandi ambako lugha ya wenyeji ni Kinandi, kuna wazungumzaji wa lugha tofautitofauti kama vile: Kiluhya, Kiluo, Kikisii na kadhalika. Wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi hawapendelei kutumia Kiswahili bali hutumia Kinandi kutekeleza shughuli mbalimbali za kibiashara bila kuzingatia kwamba kuna wazungumzaji wa lugha zingine. Ndipo utafiti huu ulilenga kueleza matumizi ya Kiswahili na sababu za matumizi haya ya lugha miongoni mwa wauza mifugo mnadani ikizingatiwa kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa na pia lugha rasmi nchini.

Kwa mujibu wa Ajzen na Fishbein (2005), mielekeo hasi au chanya kuhusu lugha fulani ni mojawapo ya sababu zinazowafanya wazungumzaji wa lugha hiyo kuwa na umilisi wa viwango tofauti. Ilibainika kuwa katika Kaunti ya Nandi, wauza mifugo mnadani wanapotumia lugha ya Kiswahili mara nyingi hawazingatii kanuni za kisarufi za lugha hiyo.

Mitazamo ya watu kuhusu dhana au kitu fulani yaweza kuathiri vitu au watu hao. Hii ina maana kuwa, mitazamo kuhusu lugha inaweza kuathiri jinsi watu wanavyoitazama lugha huyo. Ni kwa misingi hii ambapo tulilenga kufanya utafiti kuhusu matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi katika kaunti ya Nandi hasa jinsi mielekeo inavyoathiri matumizi yao ya lugha.

Kwa mujibu wa Bussman (1996:54), mielekeo ya lugha huathiri umilisi wa lugha moja kwa moja. Kwa maneno mengine, msemaji anaweza kuwa na viwango tofauti vya umilisi wa lugha kutegemea vile anavyoipenda au kuichukia lugha inayohusika. Msemaji huwa na umilisi mwingi wa lugha anayoipenda sana kwa sababu hii ndiyo lugha ambayo yeye hutumia mara nyingi katika miktadha mbalimbali ya kijamii.

Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya inayotekeleza majukumu mbalimbali (Republic of Kenya, 2010). Kulingana na Mathooko (2007), lugha ya taifa hutumika katika kuwakilisha jamii iliyo na watu wa kabila tofauti kijamii, kisiasa na vilevile kitamaduni. Kwa hivyo, kama lugha ya taifa, Kiswahili kinafaa kutumika ipasavyo kwenye shughuli tofautitofauti za kijamii na kiuchumi kama biashara. Hii ndio sababu utafiti huu ulinuia kuchunguza jinsi lugha ya Kiswahili inavyotumiwa miongoni mwa Wanandi wanaouza mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi.

## 1.2 Suala la utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza lugha ya Kinandi inavyoathiri matumizi yao ya lugha ya Kiswahili kiuchumi na kiutamaduni. Kiswahili nchini Kenya ina hadhi ya lugha ya taifa na pia hadhi ya lugha rasmi kwa hivyo lugha hii imeenea sana na ina majukumu mengi ikiwemo kushirikisha wanajamii kuingiliana kiuchumi na kitamaduni kwa ajili ya kuifaidi nchi yao.

Katika kaunti ya Nandi ambapo lugha inayotumika zaidi ni Kinandi, kuna wazungumzaji wa lugha zingine kama vile Kiluo, Kiluhya na Kikisii. Hata hivyo, kutokana na utafiti awali, ilibainika kwamba lugha ya Kiswahili aghalabu haitumiwi na wauza mifugo mnadani wanaozungumza lugha ya Kinandi kama inavyotarajiwa katika diskosi ya kijamii. Inapotumiwa watumiaji hawazingatii sarufi ya lugha ipasavyo licha ya kuwa Kiswahili kimekuwa kikifundishwa shuleni kama somo la lazima tangu mfumo wa 8-4-4 ulipoanzishwa. Suala hili linaweza kuathiri maendeleo ya Kiswahili kwa vizazi vijavyo. Kwa hivyo, kuna haja ya kuchunguza kutofautiana kwa sera ya lugha na hali halisi ya matumizi ya lugha inayotokana na mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi katika kaunti ya Nandi

## 1.3 Malengo ya utafiti

Malengo matatu yafuatayo ndiyo yaliyoongoza utafiti huu:

1. Kupambanua mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi.
2. Kubainisha mambo ambayo husababisha kuwepo kwa mielekeo mbalimbali inayohusu Kiswahili miongoni mwa wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi katika kaunti ya Nandi.
3. Kuchunguza athari za mielekeo hiyo ya lugha kwa maendeleo ya Kiswahili katika jamii ya Wanandi.

## 1.4 Maswali ya utafiti

Maswali matatu yafuatayo yaliuongoza utafiti huu:

1. Wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi katika kaunti ya Nandi wana mielekeo ipi kwa lugha ya Kiswahili?
2. Ni mambo gani yanayosababisha mielekeo mbalimbali kuhusu Kiswahili miongoni mwa wauzaji wa mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi?
3. Mielekeo tofautitofauti ya lugha inaweza kuathiri vipi maendeleo ya Kiswahili katika jamii ya Wanandi?

## 1.5 Sababu za kuchagua mada

Kulikuwa na sababu nyingi zilizochangia kuchagua mada ya utafiti huu. Moja ya sababu hizo ni makisio ya utafiti huu kuwa Kiswahili hakienziwi na watumiaji wa Kinandi katika shughuli zao za kijamii na kiuchumi; badala yake wanapendelea kutumia lugha ya kijamii ambayo ni Kinandi. Kwa mujibu wa Tsunoda (2006), lugha ya jamii ina umuhimu mkubwa. Mathalan, lugha huwa kitambulisho, huzua hisia za uzalendo na umoja na hutunza tamaduni za jamii.

Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini ambayo imefunzwa kama somo la lazima tangu mfumo wa 8-4-4 kuanzishwa nchini mwaka wa 1982. Inatarajiwa kuwa lugha inayoenziwa na wote hivyo basi wananchi wanapaswa kutumia lugha hii katika shughuli zao za kijamii. Hili ndilo jambo lingine ambalo limetuchochea kuchunguza kukinzana kwa sera ya lugha nchini na matumizi yake katika jamii.

Tunatarajia kwamba utafiti huu utawasaidia washikadau wanaojihusisha na masuala ya lugha katika kubuni mikakati inayohakikisha kwamba wanajamii wote wanafahamu na kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na kubadili mielekeo yao hasi kuhusu Kiswahili. Aidha, utafiti huu utawasaidia wadau husika kuweka mikakati ya kuboresha matumizi ya Kiswahili kwenye sekta mbalimbali kama sekta ya elimu, ya serikali na hata vyombo vya habari. Utafiti huu pia utachangia nyongeza ya marejeleo yanayohusu mielekeo katika maktaba za Kiswahili.

## 1.6 Upeo na mipaka

Utafiti huu ulikusudia kudadisi athari za mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi. Kaunti ya Nandi inapatikana nchini Kenya kwenye eneo la Bonde la Ufa na inapakana na kaunti ya Kisumu, Vihiga, Kakamega, Uasin Gishu na Kericho.

Wasailiwa katika utafiti huu walikuwa wafanyabiashara wanaouza mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi. Wahojiwa waliteuliwa kwa njia ya sampuli

makusudio. Hii ni kwa sababu aina hii ya sampuli humpa mtafiti uhuru wa kufanya uteuzi wa sampuli yenye wahusika wanaosheheni sifa anazozihitaji tu.

Utafiti huu uliwashirikisha jumla ya wasailiwa 35 walioteuliwa kimaksudi kutoka minada 7 ya mifugo katika Kaunti ya Nandi. Wasailiwa hao walijumlisha wanawake 28 na wanaume 7 wa kuanzia miaka 20 na kuendelea na walikuwa na viwango mbalimbali vya elimu (Tazama **Jedwali 3.1**).

Utafiti huu ulifanywa kuanzia mwaka 2020 hadi 2024 na ulishughulikia tu masuala yanayohusu lugha itumiwayo katika biashara ya kuuza mifugo mnadani na pia mielekeo ya wauza mifugo kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili.

## 1.7 Hitimisho

Sura hii ya utangulizi imeweka msingi wa utafiti huu kwa kuangazia vipengele vya kimsingi vya utafiti ambavyo ni: usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, na upeo na mipaka ya utafiti. Sura ifuatayo itapitia maandishi mbalimbali kuhusu suala la utafiti pamoja na kufafanua nadharia inayoongoza utafiti.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Madhumuni ya sura hii ni kupitia tafiti zilizofanywa kuhusu suala la mielekeo pamoja na kujadili historia ya mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili na maendeleo ya lugha hii nchini Kenya kuanzia kipindi cha ukoloni mpaka sasa. Hii itamwezesha mtafiti kuelewa iwapo mielekeo ya hapo awali inaweza kuathiri mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya kwa sasa. Hii ni kwa sababu moja kati ya madhumuni ya utafiti huu ni kubainisha athari ya mielekeo ya wauza mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi kwa maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya. Sura hii pia inadhamiria kufafanua misingi ya nadharia inayoongoza utafiti huu kuhusu mielekeo.

## 2.2 Yaliyoandikwa kuhusu mada

### 2.2.1 Dhana ya mielekeo

Uafiti huu ulikuwa na lengo la kwanza ambalo ni kueleza mielekeo ya Wanandi wanaouza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi. Ni muhimu kulifafanua suala la mielekeo kwa kina kwa kuwa kuna uhusiano mkubwa wa mielekeo na vitendo kwa sababu matendo ya mtu hubashiri mielekeo yake kuhusu kitu husika. Watafiti mbalimbali wameandika mengi kuhusu mielekeo. Kartz (1960) anadokeza kuwa mielekeo ya lugha ni hali ya binadamu kuienzi au

kutoienzi lugha fulani anapokabiliwa na mazingira yaliyo na mtagusano wa lugha na hivyo hali ya wingi lugha.

Webb (2000) anasema kuwa mielekeo ni kama kioo cha urazini katika jamii. Urazini huo haudhihiriki waziwazi ili kuonesha jinsi wanaotumia lugha wanavyofikiria na hupambanuliwa na kikundi cha jamii au eneo fulani. Gardner (1985) naye anasema kuwa mielekeo huhusishwa na maadili, imani za mtu na hukuza au kudumaza uteuzi wa mielekeo husika iwe chanya au hasi.

Mielekeo hujenga mitazamo ya watu kuhusu lugha au kitu fulani. Smith (1996) anasema kuwa mitazamo kuhusu lugha yaweza kusheheni hisia hasi au chanya wanazodhihirisha binadamu wajipatapo kwenye hali zinazowataka kuteua baina ya lugha yao na hali mbalimbali. Kwa hivyo, kulingana na wataalamu mbalimbali imebainika kuwa mielekeo ya binadamu kuhusu lugha au kitu fulani huwa na athari chanya au hasi kwa lugha au kitu hicho. Hivyo basi fasiri ya dhana ya mielekeo ilitusaidia kubainisha na kuchanganua mielekeo chanya na hasi ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili kupitia utumiaji wa lugha hiyo katika shughuli zao za kibiashara.

### 2.2.2 Mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili

Tafiti mbalimbali zimeshughulikia mielekeo ya watu kuhusu lugha. Mukhwana (2008) alichunguza mielekeo ya watu kuhusu lugha ili kudhihirisha hali ya lugha katika miji mikuu nchini Kenya ikiwa ni Nairobi, Kisumu na Mombasa. Utafiti huo ulibaini kwamba lugha ya Kiingereza ilienziwa ikilinganishwa na lugha

nyinginezo kama namna ya kutafuta ufanisi katika jamii. Ilibainika pia katika utafiti huu kuwa kutukuzwa kwa lugha ya Kiingereza zaidi ya lugha nyingine nchini Kenya ni hali inayozidi kudumaza maendeleo ya lugha ya Kiswahili na lugha za kienyeji. Utafiti huu ulitufaa kwa kuwa mojawapo ya malengo yetu ni kuchunguza athari ya utumiaji wa Kiswahili miongoni mwa wanaouza mifugo mnadani kwa maendeleo ya lugha hiyo katika jamii. Tofauti ya utafiti huu na wetu ni kwamba uchunguzi wetu unalenga utumiaji wa lugha mashambani na wasailiwa ni wauza mifugo mnadani pekee.

Ogola (1990) alitafiti kwa ujumla mielekeo ya watu walioelimika kuhusu utumiaji wa Kiswahili. Aligundua kuwa wasomi hawapendi kutumia Kiswahili katika shughuli rasmi wanazofanya kila siku. Kwa hivyo, mitazamo yao kuhusu Kiswahili haikuwa chanya. Vilevile, alipata kuwa upeo wa utafiti wake ulikuwa mpana mno. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa utajikita tu kwa wauza mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi. Utafiti wa Ogola unachangia utafiti huu katika kufasiri mielekeo ya wauza mifugo waliokuwa na viwango tofauti-tofauti vya elimu kuanzia shule ya msingi hadi chuo kikuu.

Mazrui (1981) alichunguza mielekeo ya Wamvita kuhusu lugha ya Kiswahili na ukubalifu wake. Alibaini kwamba Wamvita wana mielekeo hasi kuhusu Kiswahili sanifu. Kulingana na utafiti huo, Wamvita walidokeza kuwa walilazimishwa kukubali matumizi ya Kiswahili Sanifu. Licha ya hayo, utumiaji wa Kiswahili

sanifu haukubaliki katika kuendesha shughuli zao za kila siku. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa sababu tulilenga kuchunguza jinsi mielekeo ya wanaouza mifugo mnadani ambao huzungumza Kinandi katika kaunti ya Nandi inavyoathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Owalo (2014) amechunguza mitazamo ya jamii ya Waluo katika shule za msingi kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Migori. Utafiti wake uligundua kuwa Kiswahili hakitumiwi ipasavyo katika kaunti hiyo kwenye diskosi rasmi na diskosi ya jamii. Utafiti huu kama wetu ulilenga kuchunguza mitazamo kuhusu Kiswahili mashambani (kaunti ya Migori). Tofauti ni kuwa ametumia shule za msingi zilizomo Kaunti ya Migori ilhali utafiti huu ulichunguza matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wauzaji wa mifugo katika minada ya kaunti ya Nandi.

Mohochi (2011) alichunguza mitazamo ya viongozi na watu waliosoma Kiswahili Afrika Mashariki kuhusu matumizi ya Kiswahili. Utafiti huo uligundua kuwa Kiswahili kimekua na kuenea kiasi kuwa kinapambana na lugha nyingine zilizo katika viwango vya kimataifa katika enzi hizi za utandawazi. Hata hivyo, utafiti ulionyesha kuwa lugha ya Kiswahili haitapata mafanikio inavyokisiwa huko nje iwapo haitathaminiwa Afrika Mashariki. Mtafiti huyu anazidi kudokeza kuwa Kiswahili bado kinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo mielekeo ya lugha inayodhihirika katika jamii. Hivyo basi, utafiti huu unalenga kuendeleza utafiti wa Mohochi kwa kupambanua mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza

Kinandi kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi na athari zake kwa maendeleo ya Kiswahili nchini.

Kaindi (2016) alichunguza mitazamo ya wanajamii wa Kimaasai kuhusu Kiswahili katika eneo la Kitengela. Mtafiti huyu alipata kugundua kuwa Wamaasai Kitengela wana mielekeo hasi na chanya kuhusu Kiswahili kutegemea masiala mbalimbali. Utafiti huu ulilenga kupambanua jinsi lugha ya Kiswahili inavyotumiwa miongoni mwa wanaouza mifugo mnadani ambao huzungumza Kinandi katika kaunti ya Nandi.

Tafiti hizi zinachangia utafiti huu kwa kubainisha vizuri masuala mbalimbali yanayohusu mielekeo na kuboresha uelewa wetu kuhusu nadharia. Hata hivyo, tafiti hizo zimeacha pengo linalohitaji kuzibwa kwani hazikuangazia jinsi mielekeo ya wauza mifugo katika kaunti ya Nandi inavyowaathiri katika matumizi ya Kiswahili. Maelezo zaidi kuhusu historia ya mielekeo kuhusu Kiswahili nchini Kenya yatatolewa katika sehemu ya 2.2.3 na 2.2.4 ili kutusaidia baadaye katika sura ya nne kufafanua vizuri chanzo cha mielekeo hiyo na athari zake.

### 2.2.3 Maendeleo ya lugha ya Kiswahili

Kiswahili kina chimbuko lake nchini Kenya na kinapatikana kwenye familia ya lugha za Kibantu na hasa kwenye kikundi kidogo cha Wabantu wanaopatikana maeneo ya pwani ya Afrika Mashariki. Lugha zingine za pwani ambazo ni za

Kibantu ni Kitaveta, Kitaita, Kimijikenda na Kipokomo (Mbaabu, 1996). Kiswahili kinahusisha lahaja tofauti kama vile Kisiu, Kimvita, Kipate, Kivumba, Kibajuni, Kimtang`ata, Kimgao, Kichichifundi, Kimrima, Kiamu, Kipemba, Kiunguja miongoni mwa lahaja nyingine zinazozungumzwa kwenye mwambao wa bahari ya Hindi. Lahaja nyingi zinazungumzwa katika mataifa ya Kenya na Tanzania (Chiraghdin na Mnyampala, 1977; Mbaabu, 1985).

Whiteley (1969) anasema kuwa lugha hii haikubaki katika eneo hilo la upwa wa Afrika Mashariki kwa kuwa kuna sababu mbalimbali zilizochangia katika ueneaji wa Kiswahili kutoka mwambao mpaka bara. Sababu hizo ni pamoja na harakati za kibiashara, dini za kigeni, ukoloni na shughuli za kupigania uhuru.

Kihistoria, wageni walifika Mwambao wa Afrika Mashariki wakiwa na lengo la kutekeleza shughuli za kibiashara. Aidha, wenyeji wa Pwani walifanya safari kuelekea bara ili kushiriki katika shughuli za biashara na wenyeji wa bara. Wageni walipofika bara wenyeji waliwaelekeza na kuwaonesha njia walizotumia. Kwa njia hiyo, Kiswahili kilienezwa kwa sababu ni lugha iliyotumika kwenye mawasiliano katika utangamano kati ya watu wa mwambao na wa kutoka eneo la bara kwa muda mrefu hata kabla ya wageni kufika.

Muaka (2011) anasema kuwa licha ya kuwa Kiswahili kina mizizi yake katika nchi ya Kenya, lugha hii imekua na vilevile kuenea kimatumizi mpaka ikawa lugha ya

kitaifa na pia rasmi nchini Kenya na hata kufikia kiwango cha lugha ya kimataifa. Kufikia karne ya 13, Kiswahili kilikuwa kimeanza kustawi na kusambaa hadi kufikia kiwango ambapo kilianza kutumika katika shughuli za kibiashara baina ya wageni wa mwanzo waliotembelea pwani ya Afrika Mashariki wakiwemo Waarabu na Wareno na wakazi wa Kiafrika. Kwa mujibu wa Muaka, mwingiliano kati ya Kiswahili na lugha za kigeni tokea karne ya 13 uliathiri Kiswahili kupitia ukopaji wa misamiati tofauti iliyotolewa katika lugha mbalimbali ikiwa ni pamoja na  Kiarabu, Kiingereza na Kireno miongoni mwa lugha zingine. Kwa hivyo ni lugha ambayo imekua na kuendelea.

Dini za kigeni kama vile Ukristo na Uislamu nazo zilichangia pakubwa katika kueneza Kiswahili kwa wenyeji. Waarabu waliokuwa wakifundisha dini ya Kiislamu hawakuwa na budi kujifunza Kiswahili ndio waeleze mafungu ya Korani kwa kutumia lugha iliyofahamika na wenyeji. Katika upande wa dini ya Ukristo, awali wamishonari walisita kutumia Kiswahili kwa vile walikifananisha na uislamu. Hata hivyo, walilazimika  kutumia Kiswahili katika mahubiri ya Ukristo na tafsiri ya maandiko matakatifu (Whiteley, 1969).

Mwaro (2002) naye anasema kuwa Wamishenari walipowasili Afrika Mashariki walitoa msaada mkubwa katika kusambaza matumizi ya Kiswahili kwa kuhakikisha kuwa Kiswahili kimeyafikia mataifa ya Kimagharibi. Wao walichapisha vitabu vikiwemo kamusi na pia vitabu vya taaluma ya isimu katika

Kiswahili. Mwaro anaeleza kuwa wamishenari wa kutoka Ujerumani walitoa mchango mkubwa mno katika utafiti na uchapishaji kuhusu lugha ya Kiswahili.

Vipindi vitatu vya ukoloni navyo vilichangia kuenea kwa Kiswahili. Vipindi hivyo vilikuwa na athari kubwa katika maendeleo ya Kiswahili wakati wa ukoloni. Mwanzo kulikuwa na ukoloni wa Waaarabu unaohusishwa na kusambaa kwa Kiswahili. Katika kipindi hicho, watu wengi walitoka pwani kuelekea bara ambapo Kiswahili kilitumika katika mawasiliano. Pili, ni ukoloni wa Kijerumani uliokuta uimarikaji wa matumizi ya Kiswahili ambapo Wajerumani walianza kutumia Kiswahili kwenye utawala wao. Kipindi cha tatu cha ukoloni kilikuwa cha Waingereza. Ni katika kipindi hiki ambapo kazi kubwa ya kustawisha lugha ya Kiswahili ilifanyika. Kusudi la Waingereza la kuendeleza Kiswahili lilikuwa kupata wafanyakazi wa hadhi ya chini. Hawakuruhusu matumizi ya Kiswahili katika viwango vya juu (Whiteley, 1969).

Amatubi (2002) anasema kuwa jambo jingine lililosaidia kukieneza na kuendeleza Kiswahili kimataifa ni kuzinduliwa kwa idara za kufundisha masomo yanayohusu bara la Kiafrika kwenye vyuo vikuu katika mataifa ya kigeni kama vile Marekani, Uingereza na Ujerumani. Vyuo hivi vilijumuisha lugha za Kiafrika kwenye programu zao za kimasomo. Lugha hizi ikiwemo lugha ya Kiswahili ni muhimu katika vyuo hivi vinapofanya utafiti katika bara la Afrika.

Kwa mujibu wa Mwaro (2002), sanaa ya utangazaji imechangia pakubwa katika kueneza Kiswahili dunia nzima hivyo basi kuifanya kuwa lugha ya kimataifa. Vituo maarufu vya utangazaji ulimwenguni kwa mfano Voice of America(VoA), British Broadcasting Corporation (BBC), Radio China, Deutche Welle na Radio Moscow huendesha vipindi kwa kutumia Kiswahili. Vituo hivi huchangia katika kukikuza Kiswahili na kukifanya kuwa lugha ya kimataifa.

Naye Amatubi (2002) anaeleza kuwa vita vikuu vya kwanza vya dunia na vile vya pili vilikuwa na mchango wa aina yake katika kukieneza Kiswahili kwenye maeneo mapya duniani. Kwa mfano, wanajeshi walitumia Kiswahili katika mawasiliano baina yao hasa katika eneo la Afrika Mashariki na Kati. Wanajeshi hawa walipowasili maeneo mengine duniani walifikisha lugha ya Kiswahili katika maeneo hayo na kuchangia katika kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kimataifa.

Kiswahili kilitumika kama njia ya kuwaunganisha Wakenya wakati wa kupigania uhuru wa nchi ya Kenya dhidi ya wakoloni. Wakoloni walipogundua kuwa lugha ya Kiswahili ilitumika kama kiungo cha kuwaunganisha Wakenya, waliweka mikakati ya kuipiga vita ambapo walitaka lugha nyingine asilia nchini Kenya itumiwe katika ufundishaji kwenye shule za msingi kwa nia ya kusambaratisha umoja wa Wakenya. Wanaharakati wakiwemo Harry Thuku na wengine walitumia Kiswahili katika kupigania uhuru wa nchi ya Kenya. Kutokana na hali hii, Wakenya wote waliotaka ukombozi kutoka kwa wakoloni walilazimika kujifunza

Kiswahili. Kwa hivyo masiala haya ndiyo yaliyochangia kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini kote ikiwemo kaunti ya Nandi. Ni muhimu kutoa maelezo haya ya maendeleo ya Kiswahili kihistoria kwa sababu yanasaidia kuweka katika muktadha lengo la tatu la utafiti huu.

### 2.2.4 Historia ya mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya

Katika sehemu hii, tunapitia kwanza maandishi kuhusu historia ya mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya katika kipindi cha ukoloni kisha baada ya ukoloni ili kuona jinsi mielekeo hiyo inavyoathiri mielekeo ya wauza mifugo kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kaunti ya Nandi.

#### 2.2.4.1 Mielekeo ya lugha katika kipindi cha ukoloni

Sera ya lugha iliyokuweko nyakati za ukoloni nchini Kenya inaweza kuwa iliathiri mielekeo ya watu kuhusu utumiaji wa lugha mbalimbali kwa njia ambayo ni hasi au chanya. Kipindi cha ukoloni nchini Kenya kilikuwa na mchango mkubwa mno katika historia ya sera za lugha na wajibu uliotwikwa lugha tofauti.

Wamishenari wa dini ya Kikristo waliokuwa wa mwanzo wakiongozwa na Daktari Ludwig Krapf na Askofu Steere, waliendeleza Kiswahili kwa kuandika vitabu vya kufunzia habari njema kwa Kiswahili (Chiraghdin na Mnyampala,1977). Mwelekeo wa wamishenari hawa ulikuwa kuwa Kiswahili kingewawezesha katika kutangamana na Waafrika na kueneza masomo ya Kikristo miongoni mwa Waafrika nchini Kenya. Hivyo mwelekeo wao kuhusu Kiswahili ulikuwa chanya.

Wamishenari wa baadaye walionyesha mielekeo isiyopendelea utumiaji wa Kiswahili. Mielekeo hii ilisababishwa na kuhusishwa kwa lugha hii na Kiarabu ambayo ni lugha iliyokuwa pia inatumika katika mwambao wa Afrika Mashariki kabla ya kuwasili kwa wamishenari. Kulingana na Mbaabu (1991), hali hii ilifanya kutozingatia sana utumiaji wa lugha asilia katika kusambaza Ukristo katika nchi ya Kenya. Hao wamishenari walipinga Kiswahili kwa imani kuwa lugha hiyo ilikuwa ni sehemu ya lugha ya Kiarabu.

Wamishenari walizindua shule ambapo lugha ya Kiingereza ilifundishwa kama somo ilhali Kiswahili kilitumiwa katika kufundishia masomo mengine. Walipendekeza matumizi ya lugha za kienyeji kwenye madarasa ya mwanzo huku Kiswahili kikifuata baada ya hapo (Gorman 1974). Hata hivyo, wamishenari walikumbwa na hali ngumu katika kutumia lugha asilia kueneza elimu na dini ya Kikristo. Hivyo basi, Kiswahili kiliwafaa katika shughuli hizi mbili (Muthiani, 1986).

Licha ya wamishenari kukuza na kukiendeleza Kiswahili, bado mapungufu yalikuwepo katika maendeleo ya lugha hii, jambo lililofanya kuwepo kwa mielekeo hasi kati ya Waswahili na wamishenari wa jamii tofautitofauti. Hii ilisababishwa na maendelezo mbalimbali ya Kiswahili na usanifishaji upya. Kulizuka tofauti miongoni mwa wamishenari kuhusu lahaja bora katika usanifishaji wa Kiswahili. Kwa mujibu wa Mbaabu (1991), sajili iliyotumiwa

ilikuwa ya dini ya Kikristo jambo lililowafanya Waswahili wengi wa asili ya Kiislamu kutopendelea sana lugha ya Kiswahili.

Mielekeo ya wamishenari mara nyingi ilitofautiana na ile ya utawala wa kikoloni kuhusu lugha bora za kutekeleza wajibu wa kielimu. Utawala wa kikoloni ulipendelea Kiingereza tofauti na wamishenari waliopendekeza kwamba lugha za kienyeji zitumiwe. Watawala hawakutarajia utumiaji wa lugha katika kufanikisha mawasiliano pekee bali vilevile walinuia kujitegemea kwa koloni yao kiuchumi na kujistawisha wenyewe pia. Walipendelea matumizi ya Kiingereza kama njia ya kuendeleza ukoloni wa kilugha pia.

Utawala wa kikoloni haukuwa na sera maalum za lugha. Kwa mfano, watawala wengine akiwemo Hobley, ambaye alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani kipindi hicho, walipendelea kusomeshwa kwa Kiswahili na Kiingereza (Gorman, 1974). Naye Mkurugenzi wa elimu aliyeitwa Orr alipendelea matumizi ya lugha za kiasili kusomesha. Kulingana naye, kusomesha Kiswahili kulikuwa sawa na kupoteza muda, kwani mtazamo wake ulikuwa kuwa Kiswahili hakikuwa na faida yoyote kielimu. Hivyo basi, mnamo Septemba 1919, aliagiza kusomeshwa kwa Kiingereza kwenye shule zote zilizopatiwa ruzuku kutoka serikalini. Mwelekeo wake kuhusu Kiswahili na tamaduni za Wakenya uliwafanya Wakenya kuwa na mitazamo na imani kuwa Kiingereza kilikuwa na nafasi bora katika kuendeleza utamaduni vyema ikilinganishwa na lugha za kiasili (Jones, 2012).

Mnamo mwaka 1924, kamati iliyoongozwa na Phelps-Stokes ilitembelea Kenya na kulalamikia mgogoro uliokuwepo baina ya walowezi na wamishenari kuhusu sera ya lugha. Kamati hiyo ilitoa mapendekezo kadhaa mojawapo ikiwa ni matumizi ya lugha za Kiafrika zikiwemo Kiswahili, Kiluyia, Kikikuyu, Kinandi na Kidholuo. Aidha, kamati hiyo ilipendekeza kusanifishwa kwa lugha hizi na pia kutumika kielimu (Mbaabu, 2007). Baada ya muda usio mrefu, Msimamizi wa Elimu nchini alibaini kwamba ingegharimu serikali pesa nyingi mno kuchapisha nakala za kutosha katika lugha za kiasili. Kwa hivyo alipendekeza matumizi ya Kiswahili katika kufundishia shule za Kiafrika (Gorman, 1974).

Kufikia mwisho wa vita vya dunia vya pili, wakoloni walibadilisha msimamo wao wa kupendelea Kiswahili kwa mtazamo kuwa Kiswahili kingekuwa kikwazo baina ya lugha ya Kiingereza na lugha za kienyeji. Lengo la Waingereza lilikuwa ni kueneza Kiingereza miongoni mwa Waafrika. Jambo hilo liliwafanya kuiona lugha ya Kiswahili kama inayoweza kusababisha upinzani kwa vile ingeunganisha makabila mengi ya Kiafrika punde baada ya vita. Punde baada ya vita, mwelekeo huu ulifuatwa na Kiswahili kuwekwa katika kategoria moja na lugha za kiasili. Baadaye tofauti zilijitokeza kwenye silabasi kwa vile lugha tofauti kama vile Kiswahili, Kiingereza na lugha za kiasili zilitumika katika kutoa mafunzo. Hivyo basi, Wakenya walikosa usawa wa kielimu (Mukhwana, 2008). Jambo hili liliwafanya Wakenya wa kipindi hicho kuwa na mwelekeo hasi kuhusu Kiswahili.

Baada ya ripoti ya Tume ya Beecher (1942 – 1949) kutolewa, sera ya kukiendeleza Kiingereza na kudunishwa kwa Kiswahili ilipata msingi thabiti. Kwa kurejelea yaliyomo kwenye ripoti hizi, lugha ya Kiingereza na zile za kienyeji zilistahili kusisitizwa katika ufundishaji na kutwaa nafasi ya Kiswahili. Matumizi ya Kiswahili kwenye elimu yalipata pingamizi kubwa na katika mwaka 1949, tume hii ilipendekeza matumizi ya takribani lugha ishirini za kiasili kufundishia shule za mashinani. Lugha hizo ni Kimaasai, Kiborana, Kiluo, Kikisii, Kimeru, Kiluyia, Kikikuyu, Kiteso, Kitaveta, Kiturkana, Kikamba, Kigiriama, Kigala, Kipokomo, Kinandi, Kidabida, Kisuk, Kisagala, Kikisii, Kitende na Kisomali.

Aidha, Kiswahili kilipigwa marufuku kwenye shughuli zilizoendeshwa na wamishenari za kueneza elimu yenye misingi ya Ukristo kwa Waafrika (Mazrui, 1978). Hatua hii ilichukuliwa kwa vile Waswahili wengi walionekana kuwa wa dini ya Kiislamu na Kiswahili kilikuwa kimekopa baadhi ya maneno kutoka Kiarabu. Wamishenari walihusisha Kiswahili na dini ya Kiislamu, jambo lililochangia katika mwelekeo hasi wa Kiswahili katika enzi hizo.

Matumizi ya Kiswahili kufundishia yalipigwa marufuku katika shule za mjini pekee. Wakenya walivyoendelea kupata mafunzo ya Kiingereza ndivyo walivyoendelea kujifunza utamaduni wa Waingereza, jambo lililowafanya kuanza kudunisha utamaduni wao. Walijitosa katika mienendo ya Waingereza na kuona mienendo yao kama duni. Imani kuwa Kiingereza kilimfanya mtu kuwa na nafasi

bora ya kujiinua kisiasa na kiuchumi ikilinganishwa na wale wasio na ufahamu wa lugha hiyo kupitia elimu ilifanya Wakenya kuwa na mwelekeo wa kupendelea lugha ya Kiingereza na kuzidharau lugha za kienyeji walizokuwa wakizungumza.

Watawala wa kikoloni walitumia Kiswahili na lugha za kiasili kama mbinu ya kimakusudi ili kuwagawanya na kuwatenganisha Waafrika kwa urahisi. Sera za lugha katika kipindi cha kikoloni zilihakikisha kuzidi kuwepo mipaka ya lugha iliyowatenganisha na kuwagawa Waafrika na watu wengine waliokuwa wanaishi nao nchi moja (Gorman, 1974). Lugha za kiasili nchini Kenya zilichukuliwa kuwa za hali ya chini huku Kiingereza kikipandishwa cheo.

Kabla Kenya kupata uhuru, Kiswahili kilitumiwa kwenye mawasiliano baina ya waajiri, Waingereza na Waafrika waliokuwa watumishi wao. Katika mpangilio huu, mwelekeo kuwa lugha ya Kiswahili ilikuwa na hadhi ya chini ulijitokeza. Kiswahili kilichukuliwa kuwa cha wananchi wa hadhi ya chini waliokuwa na wajibu mdogo katika utawala. Kwa upande mwingine, Kiingereza kilichukuliwa kuwa lugha ya kujivunia inayozungumzwa na watu wa kiwango cha juu kwenye jamii. Jambo hili lilifanya lugha ya Kiingereza kuchukuliwa kuwa ya kifahari na ngazi ya kujipatia elimu yenye dhamana kwa wale waliobahatika kupokea elimu kwa Kiingereza (Mukhwana, 2008).

Hata baada ya utawala wa kikoloni kufikia kikomo, Wakenya wengi walizidi kuonyesha mapendeleo katika utumiaji wa lugha ya Kiingereza kwa vile lugha

hiyo imeenziwa kutoka enzi za ukoloni. Hili linadhihirisha mielekeo chanya kwa Kiingereza ambacho kimekuwa lugha rasmi tangu kuwasili kwa wakoloni hadi sasa. Kwa upande mwingine, Kiswahili kimepata mielekeo hasi kwa kuwa ni lugha ya Waafrika.

Mirianga (2014) akimnukuu Chiraghdin na Mnyampala (1977) anadokeza kuwa Wakenya walisheheni mielekeo hasi kuhusu Kiswahili na lugha nyingine za kiasili kwa sababu zifuatazo:

Kwanza, Kiingereza kilihusishwa na kundi la watu walioelimika na viongozi walioenziwa ikilinganishwa na wale ambao hawakusoma kwa kutumia Kiingereza. Kiingereza kilichukuliwa kama ngazi ya kujipatia kisomo na kuendeleza kiuchumi, kisiasa na hata kijamii. Hii inamaanisha kwamba katika nchi ya Kenya, Kiingereza kilihusishwa na nyadhifa za kuvutia na vyeo vikubwa kwenye utawala, biashara na hata kanisani. Nyadhifa hizi zilitengewa Wakenya waliosoma.

Wakoloni waliwaelekeza Wakenya kuzichukulia lugha zao kama zisizo na ustaarabu, hivyo hazikustahili kupewa nafasi ya kutumiwa katika elimu. Jambo hili liliwachochea Waafrika kutopendelea lugha zao za kiasili.

Usanifishaji wa lugha za kiasili kama vile Kiswahili ulitekelezwa na wazungu waliokuwa wa asili za Kijerumani na Kiingereza. Hili lilizua utata kwa

wazungumzaji asilia wa lugha na lahaja mbalimbali wakazichukulia lugha zao kama ngumu kusoma kutokana na tofauti katika sarufi, othografia na matamshi.

Viongozi katika shule na walimu waliwakataza wanafunzi kufanya mawasiliano katika lugha zao za kienyeji. Waliokiuka maagizo haya na kuwasiliana kwa lugha zao shuleni walipatiwa adhabu ambapo walibebeshwa mabango shuleni yaliyokuwa na maneno kama: "I am a fool" au"I dont know English" yaani "mimi ni mjinga" au "sijui Kiingereza" (wa Thiongo, 1986). Aina hii ya adhabu ilifedhehesha wanafunzi ambao walichukia kufanya mawasiliano kwa kutumia lugha asilia shuleni. Jambo hili lilichangia Wakenya kupendelea kufanya mawasiliano kwa Kiingereza ili kuepuka kufedheheshwa kwa kuongea lugha ya mama. Hili linabainisha sababu ya Wakenya kuchukia zao asilia na kupendelea lugha ya Kiingereza katika kipindi cha ukoloni. Mielekeo hii ilichochewa na mfumo wa elimu katika kipindi hicho.

#### 2.2.4.2 Mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya baada ya ukoloni

Kiingereza kilitangazwa kama lugha rasmi nchini Kenya mwaka wa 1963 baada ya Kenya kujikomboa kutoka utawala wa kikoloni. Licha ya kuwa taifa huru, Kenya ilirithi asasi za kiuchumi, kielimu, kisheria na kisiasa kutoka enzi za ukoloni. Kwa mfano, kanuni zilizowekwa wakati wa ukoloni za kuchunguza jinsi sera za lugha zingetengenezwa ziliendelea kuwepo licha ya Kenya kupata uhuru. Mtazamo kutoka wakati wa ukoloni uliendelezwa ambapo Kiingereza kiliendelea kutukuzwa huku Kiswahili na lugha za kiasili zikidharauliwa. Kwa mujibu wa

Mbaabu (1996), Kiswahili kilibaki kutambuliwa kama lugha ya taifa na pia lugha rasmi baada ya Kenya kuwa huru. Mwelekeo hasi kutoka kwa Wakenya uliendelea kubainika dhidi ya lugha ya Kiswahili na lugha zingine za kiasili huku wakiwa na mwelekeo chanya kwa Kiingereza ambacho kilikuwa kitumike kwenye sekta zote za serikali. Kiingereza kilichukuliwa kuwa lugha ya waliosoma na kupatiwa cheo cha juu ikilinganishwa na Kiswahili kwenye mashirika tofauti.

Chimerah (1998) anfafanua kwamba jamii ambazo hazikuwa za Kibantu nchini Kenya hazikukubaliana na matumizi ya Kiswahili kwa vile zilihofia zingebaguliwa kimaendeleo na matumizi ya Kiswahili. Wakati huo, wasomi na vilevile viongozi wengi hawakutilia maanani kujifunza lugha ya Kiswahili kikamilifu. Matumizi ya Kiswahili yalihusisha shughuli zisizo rasmi kama vile wakati viongozi walinuia kuleta hali ya kusikizana baina ya wananchi. Hali hii ilidhihirisha uwepo wa mielekeo chanya kuhusu Kiswahili bali uchanya huu haukuwa kamilifu.

Ingawa idadi kubwa ya Wakenya walipendelea matumizi ya Kiingereza katika kipindi cha ukoloni, hatimaye lugha hii ilitumiwa na wasomi katika kuanzisha na kuleta mapinduzi. Wakenya waligundua njama za utawala wa wakoloni kupitia masomo waliyopata kupitia lugha ya Kiingereza. Walianza kufanya bidii za kuwaunganisha Wakenya kama watu wenye maadili sawa kinyume na jinsi wakoloni walivyowachukulia.

Wakenya walioelimika walipata hamu ya kutaka ukombozi na kusahau faida walizopata kwa kukienzi Kiingereza. Hivyo basi, walijikita katika kutafuta uhuru wa kilugha ndipo wajipatie uhuru wa kisiasa. Lugha ya Kiswahili ilichukuliwa kama chombo cha kuwaleta Wakenya pamoja katika azma yao kujikomboa. Punde baada ya uhuru, mwanzilishi wa taifa la Kenya hayati Jomo Kenyatta alitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa. Lengo la tangazo hili lilikuwa kuwachochea Wakenya kubadilisha mielekeo yao hasi na kushikilia mielekeo ya kupendelea Kiswahili kama kitambulisho na kiunganishi cha jamii mbalimbali nchini Kenya. Kwa mujibu wa Kibiwott (2006), hakukubuniwa sera au sheria kimaandishi yenye kueleza namna wajibu wa lugha nchini Kenya ulivyofaa kutekelezwa. Serikali huru ya Kenya iliteua kamati na tume tofauti kwa ajili ya kudadisi na kutoa mapendekezo kuhusu mabadiliko yaliyohitajika kwenye sera za lugha nchini. Kamati au tume hizo zilikuwa na mielekeo isiyofanana kuhusu ni lugha zipi na namna ipi lugha hizo zilistahili kutumika kwenye mfumo wa elimu.

Tume ya elimu ya Ominde (1964) ilitoa mapendekezo ya matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kufundishia kutoka darasa la kwanza hadi vyuo vikuu. Tume ya Ominde ilipendekeza somo la Kiswahili lifundishwe likiwa la lazima kwenye shule za msingi kwa vile lugha hiyo ilikuwa chombo muhimu cha kuunganisha wanajamiilugha mbalimbali nchini Kenya na kama *lingua franka* ya Afrika Mashariki. Pendekezo hili linaonesha mwelekeo mzuri kuhusu wajibu wa

Kiingereza kama lugha ya kipekee kwenye mpangilio wa elimu ilhali Kiswahili kikipatiwa wajibu mwepesi wa kutambuliwa kuwa lugha ya taifa ya Kenya.

Pendekezo hili la Tume hii ya Ominde lilikataliwa kwa madai kwamba Kiswahili kingekuwa kama lugha ya kigeni kwa watoto hivyo basi ingekuwa jambo gumu kuwafundisha kwa kutumia lugha mbili za kigeni. Aidha, Tume ya Ominde ilipuuzilia mbali maoni kutoka kwa wananchi ambao walitaka Kiswahili kitumiwe kufundishia kwenye shule za sekondari. Mwelekeo wa Tume ulikuwa kuwa ingekuwa ghali na vigumu kutafsiri vitabu kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, shughuli ambayo Tume hiyo ilidai kuwa ingesababisha ufujaji wa fedha za umma. Mwelekeo wa Tume hii ulitoa mchango katika kulemaza ukuzaji wa Kiswahili.

Ripoti ya kamati ya Ukufunzi ya 1971 chini ya Mwenyekiti Bwana W.N. Wamalwa ilitoa mapendekezo kuwa Kiswahili kikuzwe na kiendelezwe. Pendekezo la kamati hii lilikuwa kutumiwa kwa Kiswahili kama lugha ya taifa. Aidha, kamati hii ilitoa pendekezo kuwa vyuo vinavyotoa maandalizi kwa wafanyikazi wa umma vianzishe kozi shadidi ili kuwapa wafanyikazi hao ufasaha wa Kiswahili. Vyuo hivi ni kama vile Taasisi ya Ukufunzi ya Serikali (GTI) na Taasisi ya Utawala (KIA) (Ripoti ya Wamalwa, 1971)**.** Mapendekezo ya kamati hii yalitiliwa maanani na serikali kwa muda mfupi kabla ya kupuuzwa. Kupuuzwa kwa mapendekezo ya tume hii kulionyesha kuwa serikali na wawakilishi wake walikuwa na mwelekeo hasi kuhusu umuhimu wa kukuza na kuendeleza Kiswahili

kama lugha ya taifa. Suala hili ni moja kati ya vyanzo vya mielekeo hasi wanayosheheni baadhi ya Wakenya wakiwemo wauza mifugo minadani katika nchi ya Kenya kufikia leo.

Kamati iliyobuniwa nchini kwa minajili ya kutoa maongozi ya lugha kielimu chini ya mwenyekiti Bw. Peter Gachathi ilitoa pendekezo kuwa lugha kuu katika maeneo ambamo shule zinapatikana zitumiwe katika shughuli ya kufundishia wanafunzi angalau katika miaka ya kwanza mitatu shuleni. Kwa upande mwingine, kamati hiyo ilipendekeza matumizi ya Kiswahili katika kufundishia shule zilizo mijini huku Kiingereza kikipendekezwa kutumika kufundishia kwenye shule za mijini ambapo kuna mchanganyiko wa watu wa asili mbalimbali. Pendekezo hili lilimaanisha kuwa lugha za kiasili, Kiingereza au Kiswahili zingetumiwa kama lugha za kufundishia kuanzia darasa la kwanza mpaka la tatu kwa kuzingatia mahali ambapo shule husika ilipatikana nchini Kenya (Chimera, 1998).

Kiswahili kilipendekezwa kama somo la kufundishwa na kutahiniwa kwa lazima mwishoni mwa masomo ya shule za msingi. Aidha, kulikuwa na pendekezo la kufundishwa na kutahiniwa kwa Kiswahili kwa lazima kwenye shule za upili. Mapendekezo haya yalibainisha mielekeo mizuri ya Kiswahili kilichotambuliwa kuwa muhimu kupitia kwenye mfumo wa elimu. Vilevile, kulikuwa na pendekezo kuwa Kiswahili kianzishwe na kifundishwe katika kiwango cha juu cha elimu

kama katika vyuo vikuu na kuandaa walimu zaidi. Jambo hili lililenga kutoa ushawishi kwa wanafunzi na walimu wawe na mielekeo ya kupendelea lugha ya Kiswahili kwa kuiona muhimu jinsi walivyoiona lugha ya Kiingereza.

Mapendekezo ya Tume ya Gachathi kuwa Kiswahili kifundishwe na pia kutahiniwa kwa lazima kwenye shule za msingi na za upili hayakutekelezwa mpaka mwaka 1985 wakati ambapo serikali ilianzisha mfumo mpya wa elimu uliojulikana kama 8.4.4. Kuchelewa kutekeleza pendekezo la kufanya Kiswahili kuwa somo la kufundishwa na kutahiniwa kwa lazima kulichangia katika kufanya idadi kubwa ya wanafunzi kuwa na mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili na kuiona kama lugha inayokosa umuhimu maishani.

Tume iliyobuniwa chini ya Daktari Mackay mwaka wa 1981 ilisheheni mapendekezo yaliyopendelea maendeleo ya Kiswahili. Kwa mfano, Tume hii ilipendekeza Kiswahili kufundishwa katika vyuo vikuu. Tume hii ilipendekeza serikali kuanzisha Idara ya Kiswahili na lugha nyingine za kiasili nchini Kenya katika chuo kikuu cha Moi ambacho serikali ilinuia kuanzisha. Tume hiyo aidha ilitoa pendekezo la Kiswahili kufanywa somo la lazima kwenye vyuo vikuu. Pendekezo hili lilizaa matunda kwani Chuo Kikuu cha Moi kilianzisha Idara ya Kiswahili mnamo mwaka 1987. Aidha, Tume ya Mackay ilipendekeza kujumuishwa kwa Kiswahili kwenye somo la Mawasiliano kwa wanafunzi wote wanaojiunga na vyuo vikuu mwaka wa kwanza.

Mapendekezo ya Tume ya Mackay kuhusu wajibu wa Kiswahili kama lugha ya taifa yaliazimia kuunda msingi thabiti wa kukuza na kuendeleza Kiswahili katika nchi ya Kenya. Uamuzi wa serikali kuidhinisha wazo la kuanzishwa kwa mfumo wa elimu wa 8-4-4 uliofanya Kiswahili kuwa somo la kufundishwa na kutahiniwa kwa lazima kwenye shule za msingi na upili ulikuwa wa manufaa katika kukuza na kuendeleza Kiswahili. Hatua hiyo ilihamasisha wengi kubadilisha mielekeo yao hasi dhidi ya Kiswahili na badala yake kuwa na mwelekeo chanya na kukionea Kiswahili fahari. Aidha, wataalamu wamechapisha aina mbalimbali ya vitabu, makala na maandishi mengine kwa Kiswahili.

Licha ya hayo, tume ya Mackay ilishikilia pendekezo la tume za awali kuwa Kiingereza kibaki kuwa lugha ya kufundishia. Kwa mujibu wa Njoroge (1990), lugha za kiasili nazo zilipendekezwa kutumika kama lugha za kufundishia katika madarasa ya mwanzoni kwenye shule za msingi japo kwenye sehemu ambapo jambo hili lingeweza kutekelezwa. Wakenya wengi ikiwa ni pamoja na wanabiashara walionyesha mielekeo mibaya kuhusu Kiswahili na lugha zingine za kiasili. Kulikuwa na chuki dhidi ya lugha za kiasili shuleni ambapo Kiingereza kilitumika badala ya lugha hizi (wa Thiongo, 1986).

Mpango wa serikali iliyokuwa mamlakani wakati huo wa kufanya Kiswahili kuwa na hadhi ya lugha rasmi uliibuliwa Aprili 1970. Kwa mujibu wa mpango huo, Wakenya wote bila kujali kabila walikuwa huru kuzungumza Kiswahili na mtu

yeyote, wakati wowote na muktadha wowote uwe rasmi au la. Aidha, Kiswahili kingetumika katika kuendesha shughuli zote za serikali. Hata wawaniaji wa nyadhifa mbalimbali kama vile ubunge, udiwani au uteuzi wowote katika serikali walihimizwa kuzungumza Kiswahili sanifu. Raia wa mataifa ya kigeni waliotaka kuwa raia wa Kenya walitakikana kudhihirisha kimaandishi au kimazungumzo uwezo wao wa kuzungumza Kiswahili. Aliyeshindwa kudhihirisha uwezo huo alikumbwa na uwezekano wa kupokonywa uraia wa Kikenya.

Kulikuwa na pendekezo la kukipa Kiswahili kipaumbele badala ya Kiingereza hasa kwenye shule za msingi na zile za upili. Serikali ilitoa ahadi ya kuanzisha kozi, kuzifadhili kozi hizo na pia kuanzisha vituo vya ufundishaji na ukuzaji wa Kiswahili.

Punde baada ya kupata uhuru, ripoti za mipango kuhusu ustawi wa kitaifa nchini Kenya zilichapishwa baada ya kila miaka mitano. Hata hivyo, kulikuwa na ripoti mbili pekee zilizoangazia suala la lugha. Ripoti ya kwanza ilikuwa ya 1979-1983 iliyotaja Taasisi ya Kiswahili kwenye Chuo Kikuu cha Nairobi iliyoanzishwa kwa lengo la kusaidia kutoa makala na maandishi toshelevu ya kielimu ya kufundisha Kiswahili shuleni (Mpango wa Maendeleo, 1979-83).

Serikali ilitoa tangazo katika ripoti ya mipango ya Maendeleo ya 1984 – 88 kwamba ingefadhili kutekelezwa kwa elimu ya kutoa mafunzo ya kuandika na

kusoma kwa watu waliopevuka kiumri, yaani elimu ya ngumbaru. Hili lilikuwa lifanyike kupitia kwenye mafunzo yaliyohusu elimu ya uraia bora, afya, ya kifamilia, na maendeleo kwenye vijiji. Lengo la mipango hii lilikuwa kushawishi Wakenya miongoni mwao wakiwa wauza mifugo mnadani dhidi ya mielekeo chanya kwa Kiswahili. Licha ya hivyo, serikali ilikosa kufuatilia mambo haya na hivyo basi taasisi iliyotarajiwa kusimamia uchunguzi, uundaji wa misamiati, maandishi na uendelezaji wa Kiswahili haikuanzishwa. Hivyo basi, mielekeo iliyokitukuza Kiingereza na kukidunisha Kiswahili ilizidi kuwepo nchini.

Nyandwaro (2015) akimnukuu Mbaabu (1996) anasema kwamba kulikuwa na mabadiliko yaliyofanyiwa katiba ya mwanzoni kuhusu sera za lugha. Kwa mfano, kulikuwa na mabadiliko katika kifungu cha 53 ambapo Kiswahili kilipatiwa cheo kipya cha kutambuliwa kama lugha rasmi kwenye bunge badala ya Kiingereza. Mabadiliko hayo yaliwakanganya wabunge kwa vile walitakikana kufanya mitihani yao kwa Kiingereza wala si Kiswahili. Hali hii ilisababisha kifungu cha 53 kufanyiwa marekebisho mengine mwaka 1975 ambapo Kiingereza na Kiswahili ziliidhinishwa kama lugha rasmi kwenye bunge.

Miaka ya 1990 ilishuhudia viongozi wakitoa hotuba zao wakitumia Kiswahili. Matumizi ya Kiswahili kwenye shughuli za kisiasa yalikipa Kiswahili hadhi mpya. Viongozi na wanasiasa waliwasiliana na umma kwa kutumia Kiswahili hasa wakati wa kampeni. Hali hii inaweza kufananishwa na wakati wa sasa ambapo

wanasiasa wanatumia Kiswahili kuhutubia umma kwenye mikutano ya kampeni na hafla za kitaifa. Aidha, mijadala kwenye bunge la kitaifa ilifanywa kwa Kiingereza na Kiswahili.

Katiba ya Kenya 2010 kifungu cha 7 ibara ya 2 inatambua Kiswahili kuwa lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya. Hii ni dhihirisho kuwa Kiswahili kimepandishwa hadhi na serikali. Kwa sasa, Kiswahili ni moja kati ya lugha pana za mawasiliano ya kimataifa kwa vile kinazungumzwa na watu wengi katika nchi takribani kumi na nne Afrika Mashariki na Kati. Kiswahili kinatumika sawia na Kiingereza katika kuendesha shughuli makanisani. Aidha, machifu na wasaidizi wao wanatumia Kiswahili wanapohudumia wananchi mashinani ambapo Kiswahili kinafahamika na wananchi wengi ikilinganishwa na Kiingereza. Hali hii inachangia kuleta mielekeo chanya kwa Kiswahili.

Kwa mujibu wa Ryanga (2001), kwa sasa Kiswahili kinatumika hadi mashinani. Hii ni kwa sababu ya mpangilio wa elimu ambao umewezesha watu kutoka jamii mbalimbali ikiwemo jamii ya Wanandi kutumia lugha ya Kiswahili.

Maandishi kuhusu mielekeo yanaonyesha kuwa hakuna utafiti uliofanywa kuhusu mielekeo ya wauza mifugo katika kaunti ya Nandi, hivyo basi, kuna haja ya kufanya utafiti huu ili kuziba pengo hilo. Vilevile inaonekana kwamba mielekeo ya Wakenya iliyokuwepo wakati wa ukoloni kuhusu lugha ya Kiswahili inaweza kuathiri maendeleo ya lugha hii wakati huu.

## 2.3 Misingi ya nadharia ya utendaji razini

Nadharia kimsingi huwa ni dira au kurunzi na huyapatia mawazo ya watafiti mwegemeo kwenye tafiti zao kiujumla. Uchunguzi huu uliongozwa na nadharia ya utendaji razini (theory of reasoned action). Nadharia hii ilibuniwa mara ya kwanza na Martin Fishbein mwaka wa 1967. Alisema kuwa binadamu ni viumbe walio na ufahamu na fikra za tabia na mielekeo yao. Hatimaye, alizipanua fikira zake akisaidiana na Icek Ajzen 1970 (Lezin, 2007) waliposema kuwa kilicho katika akili au makusudio ya tabia ya mtu ni kibashiri kabambe cha namna anavyoitikia na kutenda masuala fulani.

Kimsingi Nadharia ya Utendaji Razini huelezea uhusiano kati ya imani, mielekeo, nia ya tabia na tabia yenyewe. Kulingana na nadharia hii, kigezo cha kubashiri tabia ni lengo la tabia. Hivyo basi, vidokezo vya moja kwa moja vinavyobashiri kusudio la tabia za binadamu ni mielekeo waliyo nayo kuhusu tabia ambazo zinahusiana barabara na kanuni-nafsi (Ajzen na Fishbein 1980; Fishbein na Middlestadt, 1989; Montano na Karsprozy, 2002). Kanuni-nafsi ni hofu aliyonayo mhusika anapojiuliza kama wanaomjali watafurahishwa na mazao ya tabia au kitendo atakachotekeleza. Wanaomjali na kumzunguka ni pamoja na ndugu na jamaa zake, wateja na hata wafanyabiashara wenzake. Kwa hali hii, vijenzi vya kimsingi vya Nadharia ya Utendaji Razini ni mielekeo na ushawishi wa wanaomzunguka anayehusika; ambavyo humotisha nia ya tabia fulani na hatimaye uteuzi wa tabia halisi.

**Kielelezo 2.1: Mielekeo na utabiri wa tabia**




**Chanzo:** Ajzen & Fishbein (1980). *Understanding Attitudes and Predicting Social Behaviour*. Englewood: Prentice Hall.

Ajzen (1991) aliendeleza zaidi nadharia hii ambapo aliongeza kidokezo kingine cha kubashiri tabia alichokiita kikisio cha kudhibiti tabia (perceived behavior control) (Godin & Kok 1966). Lengo la Ajzen (1991) kubuni kikisio cha kudhibiti tabia lilikuwa ni kuimarisha zaidi uwezo wa kubashiri tabia ya Nadharia ya Utendaji Razini. Licha ya hayo, Montano na Karsprozy (2002) wanasema kuwa Nadharia ya Utendaji Razini imefaulu kuelezea tabia kwenye mazingira ya uteuzi huru. Ndiposa katika utafiti huu tulichukulia kuwa wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi katika kaunti ya Nandi wana uhuru wa kuitikia kauli mbalimbali na kujibu maswali ya wazi bila kuingiliwa kutoka upande wowote.

Kulingana na wataalamu hawa, nyongeza hii ilizua nadharia nyingine inayorejelewa na Ajzen (1991) kama Nadharia ya Tabia Ratibiwa (TPB) kikisio kikawa ndiyo mhimili mkuu. Kwa hali hii, kikisio cha kudhibiti tabia kikiwa na maana ya imani mtu anaweza kuwa nayo katika kudhibiti utendi wa tabia fulani.

Kwa kufanya hivyo, Ajzen (1991) alikuwa akitaka kubainisha mambo yaliyo nje ya udhibiti wa uhuru wa mtu ambayo yanaweza kuathiri tabia nia na tabia halisi katika hali ambapo udhibiti huru ni wa chini. Nadharia ya Tabia Ratibiwa (TPB) hufaa zaidi kupambanua tabia, tofauti na Nadharia ya Utendaji Razini. Hivyo katika hali hii, mhusika anaweza kutenda tabia fulani huku akizungukwa na mambo kadhaa ambayo yanamzuia kutenda tabia fulani (Tlou, 2009).

Tulitarajia kuwa wauza mifugo mnadani binafsi wanaozungumza Kinandi katika kaunti ya Nandi walikuwa huru katika kuteua kauli mbalimbali zilizotumika katika kupima uitikaji chanya au hasi kuhusu matumizi ya Kiswahili. Hivyo basi, uchunguzi huu ulifanywa ukielekezwa na Nadharia ya Utendaji Razini kwa vile nguzo zake zilifaa sana mada ya utafiti.

Kulingana na nadharia hii, uteuzi huru wa kitabia hubashiriwa na mielekeo kuhusu tabia inayohusika na vile anavyofikiria wanaomzunguka wanamchukulia iwapo atatekeleza tabia husika. Mielekeo ya mhusika kidesturi huathiriwa na ubainifu wa mhusika kuhusu jambo au kitu fulani. Katika utafiti huu tulijikita katika mielekeo

ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu Kiswahili. Tulichukulia kuwa itabashiri uitikaji wa tabia huru kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kati ya wauzaji wa mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi katika kaunti ya Nandi.

Wanaokubaliana na nadharia ya Utendaji Razini huamini kuwa kuna uhusiano mkubwa wa mielekeo na vitendo kwa sababu matendo ya mtu hubashiri mielekeo yake kuhusu kitu husika (Agheyisi& Fishman, 1970).

Nadharia hii hujikita katika mihimili au vijenzi vya mielekeo ambavyo ni: utambuzi lebo, tathmini ya mielekeo, tabia elekezi, uthabiti wa vijenzi vya mielekeo na kanuni nafsi.

### 2.3.1 Mielekeo ya mhusika

Kwa mujibu wa nadharia ya Utendaji Razini, sababu kuu ya mtu binafsi kuwa na nia ya kutenda ni mielekeo. Kwa hivyo mielekeo ni kitu kinachobashiri tabia aliyo nayo mtu binafsi (azma au nia). Mielekeo basi ni imani muhimu ya binadamu binafsi iamuayo kama matokeo ya tabia yake yatakuwa hasi au chanya (Ajzen na Fishbein, 1980). Ni katika msingi huu ambapo wauza mifugo mnadani wakiwa na imani chanya kuhusu Kiswahili watakuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha hiyo. Vilevile ikiwa imani yao ni hasi kuhusu matumizi ya Kiswahili basi mielekeo yao kuhusu lugha hiyo itakuwa hasi. Mhimili huu utatusaidia kupata uelewa mzuri wa

dhana ya mielekeo na hivyo kuchangia katika kutimiza lengo la kwanza la utafiti huu.

### 2.3.2 Utambuzi wa mhusika

Kidesturi mielekeo huathiriwa na ubainifu wa anayehusika kuhusu jambo au kitu fulani ambao ni utambuzilebo. Kwa mujibu wa Oppenheim (1966) binadamu muda wote huwa na mielekeo akilini mwake na hujitokeza pale anapokabiliana na anachopaswa kudhihirisha hisia za uchanya au uhasi kuhusu kitu fulani. Kwa upande wetu tulichunguza iwapo mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu Kiswahili ni hasi au chanya. Kwa mujibu wa Agheyisi na Fishman, (1970) kuna uhusiano mkubwa wa mielekeo na vitendo kwa sababu matendo ya mtu hubashiri mielekeo yake kuhusu kitu husika. Kwa hivyo utafiti huu ulichunguza jinsi wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi wanavyotumia Kiswahili ili kubaini mielekeo yao kwa lugha hiyo. Mhimili huu utachangia kutimiza lengo la kwanza la utafiti huu linalohusu kupambanua mielekeo ya wauza mifugo kuhusu Kiswahili.

Aidha, nadharia ya Utendaji Razini imeegemea katika imani kwamba mielekeo hujitokeza kwenye sehemu tatu ambazo ni hisia, fikra na vitendo (Fishbein na Ajzen, 1975). Kwa mtazamo wake anasema binadamu ana uwezo wa kuunda imani kuhusu jambo au tendo hali inayochochea kuitikia kwa namna fulani na mwishowe kudhihirika kwa vitendo au tabia fulani.

### 2.3.3 Tathmini ya mielekeo

Mielekeo huwa na kijenzi cha tathmini au kijenzi cha hisia (Michener, Delamater na Myers, 2004).Kijenzi cha tathmini kinaweza kutoa mwelekeo chanya au hasi kuhusu jambo au kitu fulani. Katika utafiti huu tulitarajia kuwa wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi wanaweza kutumia kijenzi cha tathmini cha mielekeo kupima uchanya au uhasi kuhusu matumizi ya Kiswahili. Mhimili huu utasaidia kutimiza lengo la kwanza la utafiti huu kuhusu kupambanua mielekeo wanayoshikilia wauza mifugo wa kaunti ya Nandi kuhusu Kiswahili.

### 2.3.4 Tabia elekezi

Mielekeo huhusisha maelekezo ya tabiaelekezi au tabiania kuhusu jambo au kitu. Kwa mujibu wa Ajzen na Fishbein (1980: 180), tabiaelekezi ni kipimio cha kukadiria uwezekano wa mtu kufanya kitendo ambacho kinakusudiwa. Naye Fishbein (1967) anaeleza kwamba nia au kusudi ni dhamira ya kutekeleza tabiania. Tabia elekezi husika hujengwa na mielekeo na ushawishi wa wanaomzunguka mhusika na ambao anawaona ni muhimu katika kumshaajisha kutekeleza kitendo fulani. Kwa hali hii mielekeo ya wanaowazunguka wauza mifugo mnadani iwe chanya au hasi huathiri mielekeo yao. Mielekeo tajwa ni ya kifikra na wanaowazunguka wauza mifugo mnadani ni pamoja na wanunuzi sokoni (wateja), marafiki zao, ndugu na jamaa wake na wanahofia watamchukuliaje ikiwa ataitikia kwa uchanya au uhasi. Mhimili huu utachangia kutimiza malengo ya pili na pia tatu katika utafiti huu yanayohusu kubainisha sababu za mielekeo ya wauza

mifugo wanaozungumza Kinandi kuhusu Kiswahili na athari za mielekeo hiyo katika jamii mtawalia.

### 2.3.5 Uthabiti wa vijenzi vya mielekeo

Ufahamu, tathmini na tabia ni vijenzi vya mielekeo ambavyo vinalenga kitu au jambo fulani. Hivyo tulitarajia vijenge kitu kimoja: uzima thabiti. Hata hivyo, vijenzi hivi vinatofautiana. Kama vingekuwa vinafanana, hakungekuwa na haja ya kuvitofautisha (Michener et al, 2004). Kwa hali hii kuna haja ya kuvipima na kuonyesha utofauti wake miongoni mwa wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi. Inasemekana kiwango cha juu cha uthabiti baina ya vijenzi vya ufahamu na hisia vinahusishwa na kiwango cha uthabiti wa mielekeo na hali ya kutoshawishika kwa urahisi (Chaiken & Yates, 1985). Vivyo hivyo, kiwango cha juu cha uthabiti pia huhusishwa na uhusiano shadidi baina ya mielekeo na tabia (Michener et al 2004). Utafiti huu ulibainisha uthabiti wa vijenzi vya mielekeo miongoni mwa wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuzingatia vigezo kama: mazingira, umri wa watu husika, jinsia na viwango vya elimu vya wahusika. Mhimili huu ulisaidia kutimiza lengo la kwanza la utafiti huu ambalo ni kubainisha mielekeo ya wauza mifugo mnadani katika Kaunti ya Nandi.

### 2.3.6 Kanuninafsi

Kanuninafsi ni mwelekeo wa mwanadamu kuhusu namna watu wanaomzingira wanavyomfikiria akishatekeleza tabia inayohusika. Jambo hili linajumuisha mtazamo wa aila na masahibu kuhusu matokeo ya tabia inayotarajiwa na kipimo cha umotishaji wa kutekeleza kitendo kinachohusika. Kwa sababu hiyo, katika

utafiti huu tulitarajia ushawishi wa wanaowazunguka wauza mifugo mnadani kuwa na nafasi fulani katika matumizi ya Kiswahili. Mhimili huu utasaidia kutimiza malengo ya pili na tatu ya utafiti huu ambayo ni kubainisha sababu za wauza mifugo kushikilia mielekeo fulani kuhusu matumizi ya Kiswahili na pia athari ya mielekeo hiyo kwa jamii mtawalia.

Kupitia vijenzi au mihimili hii ya mielekeo, tuliweza kubaini mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili. Kwa kuzingatia mtazamo kuhusu ufahamu wa kifikra na uitikaji kihisia, tulitarajia wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kudhihirisha tabia maalum iliyobainika kivitendo kupitia uitikiaji wa kauli tofautitofauti ambazo zilituelekeza kupima mielekeo yao kuhusu matumizi ya Kiswahili.

Ni dhahiri kwamba mihimili au vijenzi vya nadharia hii vinaweza kusaidia ufafanuzi wa suala la utafiti huu kuhusu mielekeo hivyo basi tutavitumikiza katika uchanganuzi wa data.

## 2.4 Hitimisho

Sura hii imejadili tafiti zilizofanywa kuhusu suala la utafiti na kufafanua nadharia ya utafiti. Kwa kuzingatia maelezo ya sura hii, ni dhahiri kwamba hakuna utafiti uliofanywa kuhusu mielekeo ya wauza mifugo katika kaunti ya Nandi. Pia ni wazi kwamba Kiswahili kimepiga hatua kubwa kimaenezi na kimaendeleo tokea

chimbuko lake. Hata hivyo, imedhihirika kuwa Wakenya wamejenga mielekeo hasi na chanya kuhusu Kiswahili kuanzia enzi za ukoloni hadi utawala wa sasa na hali hii inaweza kuathiri maendeleo ya lugha hii. Imedhihirika pia kwamba mihimili ya Nadharia ya Utendaji Razini ina uwezo mkubwa wa kufafanua na kuchanganua masuala yanayojadiliwa katika utafiti huu. Sura ijayo itafafanua mbinu zilizotumiwa katika utafiti huu.

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Lengo la sura hii ni kufafanua mbinu zilizotumiwa katika uteuzi wa sampuli, ukusanyaji, uchanganuzi, uwasilishaji wa data za utafiti huu pamoja na vipengele vingine muhimu. Vilevile, imeangazia masuala ya kimaadili yaliyozingatiwa katika utafiti. Taarifa hizi zitasaidia katika uchanganuzi wa matokeo ya utafiti katika sura ya nne.

### 3.2 Mbinu za Utafiti

#### 3.2.1 Muundo wa utafiti

Ritchie na Lewis (2003) wanadokeza kuwa muundo wa utafiti ni dira inayomwelekeza mtafiti kupata jawabu la maswali yake ya utafiti wake. Utafiti huu ulifanywa kwa kuzingatia jinsi uchunguzi fafanuzi ulivyo kimuundo. Huu ni muundo ambao hukadiria matokeo kwa njia ya kitakwimu na kisha tathmini hutolewa. Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kwamba lengo kuu la uchunguzi fafanuzi ni kueleza hali ya mambo jinsi ilivyo. Muundo wa uchunguzi fafanuzi ulimwezesha mtafiti kubuni maswali ambayo yaliibua data aliyohitaji kuhusu hali ya mielekeo ya wauza mifugo mnadani. Pia ulimwezesha mtafiti kutambua wasailiwa waliohusishwa na njia ambazo zilitumika katika ukusanyaji wa data.

Uchunguzi huu ulizingatia mikabala ya kitakwimu na kimaelezo inayohusisha kwa upande mmoja maelezo na utoleaji wa sababu kitakwimu. Wasailiwa walitarajiwa kujibu kauli zote zilizochaguliwa baada ya uchunguzi wa awali huku wakibainisha utambuzi wa mielekeo kuhusu matumizi ya Kiswahili katika shughuli zao za kibiashara.Vigezo vilivyohusishwa ni viwango vya elimu, umri, jinsia na lugha walizofahamu wasailiwa.

### 3.2.2 Mahali pa utafiti

Uchunguzi huu uliendelezwa katika masoko mbalimbali katika kaunti ya Nandi. Kaunti ya Nandi inapakana na kaunti ya Kisumu, Kakamega, Uasin Gishu, Vihiga na Kericho (Tazama **Kiambatisho cha 6**). Kaunti hii iliteuliwa kwa sababu ina wazungumzaji asilia wa Kinandi na kuna wazungumzaji wa lugha zingine kama Dholuo, Kikisii na Kiluyia ambao husababisha kuwa na uwingi lugha.

Sababu nyingine ya kuchagua kaunti ya Nandi kama eneo la utafiti huu ni kuwa mifugo huchukua nafasi kubwa katika utamaduni wa jamii ya Wanandi. Uchunguzi wa utumiaji wa Kiswahili kati ya wanaouza mifugo mnadani utatupa picha halisi ya shughuli za kijamii na kiuchumi, imani na itikadi ambazo zimefungamana na ufugaji na uuzaji wa mifugo katika kaunti ya Nandi na hivyo kuelewa matumizi ya Kiswahili katika kaunti hii. Ufugaji wa mifugo ni shughuli mojawapo ya kiuchumi katika kaunti ya Nandi ambapo uuzaji na ununuzi wa mifugo ni shughuli iliyo na umuhimu katika jamii. Matumizi ya Kiswahili katika kunadi mifugo huleta taathira halisi ya mabadiliko ya lugha na matumizi yake ili

kupeana ujumbe muhimu kuhusu uchumi wa jamii na uwezekano wa kujuza sera za kuinua sekta hii.

### 3.2.3 Kikundilengwa

Kundi lengwa ni jumla ya watu, matukio, taasisi au vitu vyote vinavyohusishwa katika utafiti. Kwa hivyo, kundi lengwa katika utafiti huu ni wauza mifugo mnadani walio na ujuzi wa lugha ya Kinandi na wanaoweza kuzungumza Kiswahili. Walengwa hawa walisaidia kutoa taarifa zilizohitajika katika utafiti huu kuhusu matumizi ya Kiswahili mnadani.

### 3.2.4 Uteuzi wa sampuli

Kothari (2004) anaeleza kuwa sampuli ni kikundi kidogo cha wanaosailiwa ambao huteuliwa kutoka kwenye kikundi kikubwa anachotumia mtafiti kupata data inayomwezesha kupata matokeo na mahitimisho. Sampuli katika utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia sampuli kimakusudi. Hatua hii ilifanikisha kupata walengwa binafsi kwa minajili ya kuwahoji. Tulichunguza wauzaji mifugo katika minada yote saba ikiwemo Lemook, Kabiyet, Chepterit, Labuiywo, Kibwareng`, Kaptumo na Chebarus kwa kuwateua walengwa watano kutoka kila mnada huku tukizingatia umri, jinsia, viwango vyao vya elimu pamoja na lugha ya mzungumzaji. Hii ni kwa sababu minada katika kaunti ya Nandi ni michache. Tungechunguza mnada mmoja pekee hatungeweza kupata data ya kutosha ambayo ingetuwezesha kutoa kauli za kijumla kuhusu hali ya matumizi ya lugha miongoni mwa wauza mifugo. Mtafiti aliwahoji washiriki 35. Idadi hii ilikisiwa kuwa

toshelevu katika kupata data ya kutosha. Uteuzi wa sampuli ulifanywa kama ifuatavyo:

**Jedwali 3.1: Uteuzi wa Sampuli**

| **KIGEZO** | **MIAKA** | **IDADI** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|
| Umri | 20 – 30 | 7 | 35 |
| | 31 – 40 | 15 | |
| | 41 – 50 | 8 | |
| | 51 na Zaidi | 5 | |
| Elimu | Shule ya Msingi | 13 | 35 |
| | Shule ya Upili | 14 | |
| | Vyuo anuai | 7 | |
| | Vyuo vikuu | 1 | |
| Jinsia | Kiume | 28 | 35 |
| | Kike | 7 | |
| Lugha | Kiswahili | 7 | 35 |
| | Kinandi | 16 | |
| | Kiingereza | 0 | |
| | Kuchanganya zote | 12 | |

### 3.2.5 Utafiti wa awali

Utafiti wa awali ulifanywa katika kaunti ya Uasin Gishu. Hii ni kaunti iliyo jirani na kaunti ya Nandi. Kaunti hii ilichaguliwa kwa sababu ina sifa sawa na za kaunti ya Nandi. Utafiti huu wa awali ni muhimu kwa sababu ulisaidia katika kuona

changamoto ambazo tungeweza kukumbana nazo katika utafiti halisi hasa kuhusu vifaa vya ukusanyaji wa data. Baada ya utegemeo na uthabiti wa vifaa husika kudhibitika, utafiti kamili ulifuata.

### 3.2.6 Mbinu za ukusanyaji data

Mugenda na Mugenda (2003) wanaeleza data kama taarifa zote anazokusanya mtafiti kwa minajili ya kufanya utafiti wake. Mbinu za ukusanyaji data hutumiwa na mtafiti ili kupata data ya utafiti. Ukusanyaji data ulifanyika nyanjani na wazungumzaji asilia wa lugha ya Kinandi walipewa hojaji kujaza na kupewa fursa ya kueleza mitazamo yao kuhusu Kiswahili. Hojaji ilitumiwa kwa sababu iliweza kukusanya data kutoka kwa idadi kubwa ya wasailiwa kwa muda mfupi.

Hojaji ilikuwa na sehemu nne: kwanza ni habari za kimsingi za mtafitiwa; sehemu ya pili ilishughulikia mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu utumiaji wa Kiswahili katika kaunti ya Nandi; sehemu ya tatu ililenga mambo ambayo husababisha mielekeo mbalimbali kuhusu Kiswahili baina ya wauza mifugo minadani wanaozungumza Kinandi; sehemu ya nne iliangazia athari ya mielekeo hiyo ya lugha kwa maendeleo ya Kiswahili katika jamii ya wazungumzaji wa Kinandi. Pia kwa kutumia hojaji, tuliweza kulinganisha majibu ya wahusika mbalimbali ili kukadiria ukweli.

Hojaji hiyo ilikuwa na aina mbili ya maswali ambayo ni wazi na funge. Kwenye hojaji funge, wasailiwa walihitajika kuteua majibu kutoka majibu waliyopewa.

Hili lilimsaidia mtafiti katika kuwaelekeza wasailiwa kwenye majibu mahususi. Aidha, njia hii iliwawezesha wasailiwa kuzijaza zile hojaji haraka pasipo kuchoka. Hojaji wazi iliwawezesha wasailiwa kutoa maoni yao kuhusu walichoulizwa. Hojaji kuwa na maswali wazi na funge ilimsaidia mtafiti kupata data nzuri iliyomsaidia kujua na kuelewa vyema suala alilolichunguza.

Kushiriki ni mbinu nyingine tuliyotumia kukusanya data. Kushiriki kulihusu mtafiti kujihusisha na utendaji wa shughuli inayofanywa na wanajamii na washikadau (Bucker, 2018). Njia ya kushiriki huwezesha mtafiti kuthibitisha habari zilizokusanywa kwa njia ya hojaji. Hii ni kwa sababu mtafiti na mtafitiwa huja pamoja. Tulishiriki katika uuzaji na ununuzi wa mifugo mnadani huku tukinakili data muhimu iliyotuwezesha kubaini mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi.

Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya **3.2.4** kuhusu uteuzi wa sampuli, mtafiti alikusanya data kutoka kwa wasailiwa 35 waliojumuisha wanaume 28 na wanawake 7 walioteuliwa kimaksudi kutoka kila mnada. Wasailiwa hao walitoka katika minada 7 ya kaunti ya Nandi ambapo mwanamke 1 na wanaume 4 waliteuliwa kutoka kila mnada. Mtafiti pia aliwateua kimaksudi wasailiwa hao kwa kuzingatia kwamba waliwakilisha vipindi tofauti vya umri na viwango tofauti vya elimu kama ilivyoonyeshwa katika **Jedwali la 3.1.**

### 3.2.7 Uchanganuzi wa data

Baada ya mtafiti kukusanya data kupitia hojaji na kushiriki, uchanganuzi wa data hizo ulifanywa kwa kuongozwa na malengo ya uchunguzi. Data kutoka kwa hojaji ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kijarabati ili kubainisha uchanya au uhasi wa mielekeo ya wauza mifugo mnadani kwa lugha ya Kiswahili. Ili kuwa na uhakika kuhusu milelekeo chanya au mielekeo hasi, tulitoa maelezo na pia kushirikisha programu ya Uchanganuzi wa data za Kitakwimu za Sayansi Jamii (Statistical Package for Social Sciences - SPSS). Maelezo yalisaidia kufafanua sababu za mielekeo na athari zake ilhali programu ya SPSS ilisaidia katika kufanya hesabu ya idadi ya wasailiwa waliokuwa katika kategoria mbalimbali. Data ya hojaji hizi ilihusu zaidi kubaini mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili.

### 3.2.8 Uwasilishaji wa data

Baada ya kuchanganua data, matokeo yaliwasilishwa kwa mbinu ya kimaelezo na kijarabati. Njia za kijarabati ambazo tuliweza kuzitumia ni pamoja na baa grafu, pai chati na jedwali za frikwenzi. Hii ilisaidia kupambanua mielekeo mbalimbali ya wauza mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi na jinsi mielekeo hiyo inavyoweza kuathiri maendeleo ya Kiswahili kwa vizazi vijavyo. Kisha matokeo ya uchunguzi yaliegemea kutimiza madhumuni na kujibu maswali ya uchunguzi kulingana na nadharia ya utafiti huu.

Kimuundo, tasnifu hii imewasilishwa kupitia kwa sura tano na kuongozwa na malengo matatu mahsusi kwa kuzingatia masharti ya Idara ya Kiswahili na Shule

ya Sheria, Fani na Sayansi za Jamii katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Tunafahamu kwamba katika Shule hii, kuna miundo miwili tofauti inayofuatawa katika kuandika tasnifu. Katika muundo wa kwanza, sura ya kwanza huwa inahusu utangulizi wa jumla wa utafiti; sura ya pili hutimiza lengo la kwanza; sura ya tatu hutimiza lengo la pili; sura ya nne hutimiza lengo la tatu; na sura ya tano huhitimisha utafiti. Lakini katika muundo wa pili wa tasnifu, sura ya kwanza inahusu utangulizi, sura ya pili ni mapitio ya maandishi na nadharia, sura ya tatu ni mbinu za utafiti, sura ya nne ni matokeo ya utafiti na tahakiki, na sura ya tano ni mahitimisho.

Katika tasnifu hii, tumefuata muundo wa pili ambao ndio unaingiliana vizuri zaidi na suala la utafiti huu. Hivyo basi, sura ya kwanza ni utangulizi; sura ya pili inapitia maandishi kuhusu suala la utafiti ili lieleweke katika muktadha wa kihistoria na pia inafafanua nadharia iliyoongoza utafiti huu; sura ya tatu inafafanua mbinu za uafiti; sura ya nne inawasilisha, inachanganua na kujadili data ya utafiti ili kutimiza lengo la kwanza, la pili na la tatu la utafiti; na sura ya tano inahitimisha utafiti kwa kutoa muhtasari wa matokeo na kueleza changamoto na mapendekezo ya utafiti huu.

### 3.3 Maadili ya utafiti

Mtafiti aliomba barua ya kumruhusu kufanya utafiti huu kutoka kwa Shule ya Masomo ya Shahada za Juu Chuoni na pia kutoka kwa Kamisheni ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (NACOSTI) (Tazama **Kiambatisho cha 5**).

Mtafiti alijitambulisha kwa wasailiwa waliokuwa nguzo muhimu katika kupata data lengwa nyanjani. Mtafiti aliwaeleza kuwa utafiti huu utakuwa muhimu katika kuchangia tafiti za lugha na isimu kwenye vyuo vikuu na katika eneo pana la kiusomi. Aidha, mtafiti aliwajulisha waliohojiwa kwamba walikuwa na hiari kushiriki au kutoshiriki katika kujibu maswali kwenye hojaji baada ya kujulishwa awali natija za utafiti huu. Mtafiti aliwaheshimu wasailiwa jinsi inavyoagizwa kwenye sheria za utafiti wa nyanjani ikiwa ni pamoja na kubana majina ya wahojiwa wakati wa kufanya utafiti. Vilevile, asili za data zote zilizotumika zilirejelewa, kuhifadhiwa na kunukuliwa kwenye marejeleo.

## 3.4 Hitimisho

Sura hii imefafanua vipengele mbalimbali vya mbinu zilizotumiwa kufanyia utafiti huu. Maelezo hayo yalimsaidia mtafiti kupata wasailiwa na data mwafaka ambayo imewasilishwa, ikachanganuliwa na kujadiliwa kwa kina katika sura ifuatayo ili kutimiza malengo ya utafiti huu.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI WA MATOKEO NA MJADALA KUHUSU MIELEKEO YA WAUZA MIFUGO

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha, inachanganua na pia inajadili data iliyokusanywa kuhusu mielekeo ya wauza mifugo kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi. Matokeo ya uchanganuzi huo yalisaidia kutimiza malengo matatu yaliyoongoza utafiti huu ambayo ni: kupambanua mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kwa lugha ya Kiswahili katika kaunti ya Nandi; kubainisha mambo ambayo husababisha mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu lugha ya Kiswahili na kuchunguza athari ya mielekeo hiyo ya lugha kwa maendeleo ya Kiswahili katika jamii hii. Mpangilio katika sura hii unahusisha mada kubwa na ndogo zinazotokana na hayo malengo matatu.

## 4.2 Uwasilishaji wa matokeo

Mielekeo imejadiliwa kwa kuongozwa na misingi ya Nadharia ya Utendaji Razini na pia kwa kuangazia nafasi ya Kiswahili kama lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya. Nadharia hii inafafanuliwa na Ajzen na Fishbein (1980) wanaosema kuwa iwapo binadamu analienzi jambo fulani, atadhihirisha mwelekeo chanya ilhali mwelekeo wake utakuwa hasi iwapo halienzi jambo hilo. Nadharia hii ilitumika

kubainisha sababu za mielekeo waliyoshikilia wauzaji mifugo mnadani kuhusu lugha ya Kiswahili.

Sampuli kielelezo ni minada ya mifugo pekee kwenye masoko ya Lemook, Kabiyet, Chepterit, Maraba, Kibwareng`, Kaptumo na Chebarus, yote yanapatikana katika kaunti ya Nandi. Walengwa katika utafiti huu ni wafanya biashara wanaonadi mifugo na ni wale wanaozungumza Kinandi pekee. Wauza mifugo hawa waliteuliwa kimakusudi ambapo vigezo vya umri, jinsia na kiwango cha elimu vilizingatiwa. Wasailiwa hawa walichaguliwa kwa kuwa wao ndio wanaohusika sana katika muktadha huu. Kwa hivyo, matokeo ya utafiti huu yatakuwa maelekezo mazuri kuhusu hali ya maendeleo ya Kiswahili mashinani hasa kwenye sekta ya kibiashara mnadani.

### 4.2.1 Wasailiwa katika utafiti

Uchunguzi huu ulilenga jumla ya wasailiwa 35 walioteuliwa kimaksudi kutoka jamiilugha ya Kinandi katika kaunti ya Nandi. Wao walikuwa wasailiwa watano kutoka kila soko. Jinsia zote mbili za kike na kiume zilisailiwa. Wasailiwa walijaza hojaji zote na kuzirejesha kwa mtafiti. Wale waliokuwa na changamoto za kujaza hojaji walielekezwa ipasavyo. Wasailiwa waliulizwa maswali yaliyolenga kutimiza malengo ya utafiti huu ambayo tayari yamebainishwa katika sehemu ya 4.1.

Wahusika wote walishiriki kujaza hojaji ambapo maswali fuatilizi yalitumiwa kwa ajili ya kupata mielekeo waliyokuwa nayo kuhusu Kiswahili. Kama anavyodai Wendo (2009), watu wengi huchukulia Kiswahili kama lugha iliyo na msamiati mgumu kuelewa. Baadhi ya wasailiwa waliongozwa katika kujaza hojaji kwa sababu walisema kuwa Kiswahili ni kigumu.

Vigezo vifuatavyo ndivyo vilivyochunguzwa: Umri wa wahusika, viwango vyao vya elimu, jinsia na lugha wanazozifahamu. Sifa za kimsingi za wasailiwa walioshiriki kwenye utafiti zimeonyeshwa katika **Jedwali 3.1** lililo katika sura ya tatu sehemu ya **3.2.4** (Uteuzi wa Sampuli).

### 4.2.2 Uchanganuzi wa mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu lugha ya Kiswahili

Uchanganuzi wa data ulidhihirisha jinsi wahusika walivyotoa majibu yao kuhusu mielekeo. Lengo la kwanza la uchunguzi huu ni kubaini mielekeo ya wauza mifugo kuhusu lugha ya Kiswahili. Mielekeo yao ilipimwa kwa kuzingatia kauli za hojaji ya Likert iliyo na vibadala vitano: 'nakubali kabisa, nakubali, sina hakika, sikubali, sikubali kabisa.' Vibadala hivi vinalingana na kauli kumi za wauza mifugo.

Wauza mifugo waliombwa kuchagua jawabu moja ambalo linaonyesha mwelekeo wa mtafitiwa kuhusu lugha ya Kiswahili. Wanaoshikilia nadharia ya utendaji

razini wanaamini kuwa iwapo binadamu analienzi jambo fulani, mwelekeo wake kwa jambo hilo utakuwa chanya ilhali kama halienzi jambo ataonesha mwelekeo hasi (Ajzen na Fishbein, 1980). Kwa hoja hii majibu ya ‘nakubali kabisa’ na ‘nakubali’ yanaonyesha mielekeo chanya na ikiwa hapendi hudhihirisha mwelekeo hasi kwa kusema ‘sipendi’ na ‘sipendi kabisa.’

Maswali ya viwango yaliyoulizwa wauza mifugo mnadani ili kutumiwa katika kupima uchanya au uhasi wa mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu lugha ya Kiswahili yanapatikana kwenye **Kiambatisho 3** ambacho tumeona ni bora kudondoa kauli zake hapa. Zifuatazo basi ni kauli kumi ambazo wauza mifugo walipewa ili kuonyesha viwango vya ukubalifu wao**:**

1. Naipenda lugha ya Kiswahili.

2. Lugha ya Kiswahili ina manufaa katika maisha kwa jumla.

3. Naridhishwa na nafasi ya Kiswahili nchini.

4. Lugha ya Kiswahili hutumika kwenye shughuli tofauti za kijamii wakati wowote.

5. Kiswahili ni kigumu mno.

6. Natumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na wenzangu mnadani.

7. Lugha ya Kiswahili ina manufaa kwangu kama Mkenya

8. Siridhishwi na jinsi Kiswahili kilivyofunzwa shuleni.

9. Lugha ya Kiswahili ni lugha inayostahili kutumika katika mawasiliano yetu ya kila siku.

10. Ujuzi wa lugha hii ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa hutegemea mazingira alimokulia mzungumzaji.

Jedwali linalofuata linaonesha mtawanyiko wa idadi ya kauli zilizotolewa na wasailiwa ili kujibu maswali yaliyotajwa hapo juu:

**Jedwali 4.1: Majibu ya maswali ya viwango vya mielekeo kwa wauza mifugo mnadani**

| | **Nakubaliana kabisa (1)** | **Nakubaliana (2)** | **Nakataa (3)** | **Nakataa kabisa (4)** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Swali la 1** | 3 | 6 | 7 | 19 | 35 |
| **Swali la 2** | 9 | 13 | 10 | 3 | 35 |
| **Swali la 3** | 10 | 13 | 7 | 5 | 35 |
| **Swali la 4** | 15 | 8 | 11 | 1 | 35 |
| **Swali la 5** | 20 | 6 | 4 | 5 | 35 |
| **Swali la 6** | 4 | 11 | 7 | 13 | 35 |
| **Swali la 7** | 15 | 9 | 10 | 1 | 35 |
| **Swali la 8** | 18 | 5 | 5 | 7 | 35 |
| **Swali la 9** | 15 | 5 | 4 | 11 | 35 |
| **Swali la 10** | 20 | 10 | 5 | 0 | 35 |
| **Jumla %** | **187 = 53.4% (chanya)** | | **163 = 46.6% (hasi)** | | |

Katika utafiti huu uliotumia mizani ya Likert, kauli kumi zilitumiwa katika kupima mielekeo ambapo kauli zilizo na uchanya ni 8 na zenye uhasi ni 2 (kauli ya 5 na 8). Kila kauli iliibua majibu ya kukubali na kukataa. Katika kauli zilizo na uchanya, majibu ya "Nakubaliana kabisa" na "Nakubaliana" yaliashiria mwelekeo chanya ilihali majibu ya "Nakataa" na "Nakataa kabisa" yaliashiria mwelekeo hasi. Lakini katika kauli zilizo na uhasi (ya 5 na 8), majibu ya "Nakubaliana kabisa" na "Nakubaliana" yaliashiria mwelekeo hasi ilihali majibu ya "Nakataa" na "Nakataa kabisa" yaliashiria mwelekeo chanya. Hivyo basi, majibu yaliyopakwa rangi ya kijivu yaliashiria mielekeo chanya ya wauza mifugo ilihali majibu yasiyopakwa rangi yaliashiria mielekeo hasi. Hii inadhihirisha kuwa asilimia **53.4%** ya wauza mifugo mnadani wana mielekeo inayopendelea lugha ya Kiswahili, yaani mielekeo chanya ilihali asilimia **46.6%** ya wauza mifugo mnadani wana mielekeo isiyopendelea Kiswahili, yaani mielekeo hasi.

#### 4.2.2.1 Matumizi ya lugha na mielekeo kuhusu Kiswahili

Swali lililoulizwa wasailiwa lilikuwa: Je, ni lugha ipi unayopenda kutumia katika kunadi mifugo mnadani. Jedwali lifuatalo linadhihirisha matokeo yao.

**Jedwali 4.2: Matumizi ya lugha na mielekeo kuhusu Kiswahili**

| LUGHA | IDADI YA WASAILIWA | ASILIMIA |
|---|---|---|
| Kiswahili | 7 | 20% |
| Kinandi | 16 | 45.7% |
| Kuchanganya Lugha | 12 | 34.3% |
| Jumla | 35 | 100% |

Kulingana na matokeo ya utafiti, ilidhihirika kuwa wasailiwa saba ambao ni asilimia 20% hupendelea Kiswahili katika biashara yao ya kunadi mifugo mnadani. Wasailiwa 16 ambao ni asilimia 45.7% wanapendelea Kinandi na wale wanaopendelea kuchanganya lugha zote wanazofahamu ni wasailiwa 12 ambao ni asilimia 34.3%.

**4.2.2.2 Umri wa wauza mifugo na mielekeo kuhusu Kiswahili**

Wasailiwa waliulizwa kutaja umri zao. Jedwali lifuatalo lilidhihirisha matokeo ya umri wa wasailiwa.

**Jedwali 4.3: Umri wa wasailiwa katika utafiti**

| | UMRI (MIAKA) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **20 – 30** | **31 – 40** | **41 – 50** | **50 na zaidi** | **Jumla** | **Asilimia** |
| **LUGHA** | **Kiswahili** | 5 | 1 | 1 | 1 | 8 | 22.9% |
| | **Kiingereza** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Kinandi** | 1 | 3 | 4 | 8 | 16 | 45.7% |
| | **Kuchanganya Zote** | 3 | 5 | 2 | 1 | 11 | 31.4% |

Kwa mujibu wa jedwali kuhusu umri wa wasailiwa, wasailiwa wa umri kati ya 20 na 30, watano hupendelea Kiswahili, hakuna anayependa kutumia Kiingereza na mmoja hupenda kutumia Kinandi na wa kuchanganya lugha zote ni watano. Wasailiwa waliokuwa na umri wa kati ya 31 na 40, mmoja hupendelea Kiswahili, hakuna anayetumia Kiingereza, watatu hutumia Kinandi na wanaopenda kuchanganya lugha zote ni watano. Kuhusu wasailiwa wa umri wa kati ya 41 na 50, wasailiwa wanne hupendelea Kinandi, mmoja hutumia Kiswahili na wanaopenda kuchanganya lugha ni wanne. Kwa wasailiwa wa umri wa miaka hamsini na zaidi, mmoja hupendelea Kiswahili, hakuna anayependa kutumia Kiingereza mnadani, wanane hutumia Kinandi na mmoja hupendelea kuchanganya lugha zote. Kwa ujumla, asilimia 22.9% ambao ni wanane hupenda kutumia Kiswahili, asilimia 45.7% hutumia Kinandi na asilimia 31.4% hupendelea kuchanganya lugha zote. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa umri huathiri matumizi ya lugha baina ya wanajamii.

#### 4.2.2.3 Viwango vya elimu na mielekeo kuhusu Kiswahili

Wauza mifugo mnadani wana viwango tofauti vya elimu ambapo kuna wale waliosoma hadi vyuo vikuu, kuna wale waliofika vyuo anuai na vilevile kuna wale waliomalizia shule za msingi na sekondari. Matokeo ya mielekeo yao ni ifuatavyo:

**Jedwali 4.4: Viwango vya elimu**

| | KIWANGO CHA ELIMU | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **LUGHA** | | **Shule ya Msingi** | **Shule ya Upili** | **Vyuo Anuai** | **Vyuo Vikuu** |
| | **Kiswahili** | 2 | 3 | 1 | 1 |
| | **Kinandi** | 8 | 7 | 3 | 0 |
| | **Kiingereza** | 0 | 0 | 1 | 0 |
| | **Kuchanganya zote** | 3 | 4 | 2 | 0 |
| | **Jumla** | 13 | 14 | 7 | 1 |
| | **Asilimia** | 37.1 | 40 | 20 | 2.9 |

Kulingana na matokeo ya utafiti, jumla ya wasailiwa waliofika shule za msingi ni 13; kati yao wawili hupendelea Kiswahili mnadani, wanane wanapendelea Kinandi, hakuna anayependelea Kiingereza na wa kuchanganya lugha zote ni watatu. Wasailiwa waliofika shule ya upili ni 14; kati yao wanaopendelea Kiswahili ni watatu, wanaopendelea Kinandi ni saba, hakuna wa kupendelea Kiingereza na wale wa kuchanganya lugha zote ni wanne. Wasailiwa waliofika vyuo anuwai ni saba; kati yao mmoja hupendelea Kiswahili, watatu wanapendelea Kinandi, mmoja hupendelea Kiingereza na wawili hupendelea kuchanganya lugha zote. Kati ya wasailiwa wote, mmoja alikuwa na elimu ya kiwango cha chuo kikuu. Yeye alipendelea kutumia Kiswahili katika kunadi mifugo mnadani. Asilimia ya wasailiwa waliosoma hadi shule ya msingi, shule ya upili, vyuo

anuwai na chuo kikuu ni 37.1%, 40%, 20% na 2.9% mtawalia. Hivyo basi, wauza mifugo wengi walisoma hadi shule ya msingi na ya upili.

#### 4.2.2.4 Jinsia na mielekeo kuhusu Kiswahili

Kigezo cha jinsia ya wasailiwa kilitiliwa maanani kwenye utafiti huu ili kuhakikisha kuwa ushirika wa wasailiwa kijinsia katika sekta ya biashara ulikuwa sawa.

Jedwali lifuatalo lilidhihirisha matokeo ya utafiti kuhusu suala la jinsia.

**Jedwali 4.5: Jinsia**

| Jinsia | Idadi | Hisia Chanya | Asilimia | Hisia Hasi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kiume** | 28 (80%) | 18 | 64.3% | 10 | 35.7% |
| **Kike** | 7 (20%) | 6 | 85.7% | 1 | 14.3% |

Wanaume waliosailiwa ni 28 na kati yao wanaume 18, sawa na asilimia 64.3%, walidhihirisha hisia chanya kwa Kiswahili, nao waliodhihirisha hisia hasi ni 10, sawa na asilimia 35.7%. Waliosailiwa wa jinsia ya kike ni 7, kati yao sita, sawa na asilimia 85.7%, walidhihirisha hisia chanya na mmoja, sawa na asilimia 14.3%, akadhihirisha hisia hasi.

## 4.3 Mjadala kuhusu mielekeo ya wauza mifugo

Sehemu hii inajadili matokeo ya uchanganuzi wa data iliyokusanywa kuhusu mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili.

### 4.3.1 Mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi

Mojawapo ya malengo ya utafiti huu ilikuwa kubaini mielekeo walio nayo wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi. Makisio yetu yalikuwa kwamba, huenda wauza mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Hii huenda ikawa sababu inayoweza kuwafanya kutotumia Kiswahili katika shughuli zao za kibiashara licha ya Kiswahili kuwa lugha ya taifa nchini.

Upo uhusiano mkubwa kati ya mielekeo ya lugha ya jamii za wafugaji na maisha yao ya kiasili na mazingira wanamokaa. Wafugaji mara nyingi huzithamini sana lugha zao asilia kwa sababu lugha hizo huwatambulisha kitamaduni na pia huwawezesha kuwasilisha maarifa yao kuhusu uhifadhi wa mazingira na ufugaji. Hata hivyo, kuna sababu mbalimbali ambazo zinaweza kuathiri mielekeo ya wafugaji hao kuhusu utumiaji wa lugha. Sababu hizo ni pamoja na umri, viwango vya elimu, jinsia, maendeleo ya kisasa, sera za serikali na uaminifu kwa lugha asilia. Wanaisimujamii kama vile Baker (1992:106) wanasema kwamba mielekeo kuhusu lugha huathiriwa kwa kiasi kikubwa na sababu za kijamii, kuliko mielekeo ya kisaikolojia.

Kulingana na Ajzen na Fishbein (2005), wazungumzaji wa lugha wanaweza kuwa na mielekeo isiyofanana kuhusu lugha, yaani, wapo watu ambao wana mielekeo chanya na wengine hasi. Suala la kuwepo kwa mielekeo chanya au hasi kuhusu

lugha ndilo lililochunguzwa kwenye utafiti huu ili kubaini kweli iwapo lugha ya Kiswahili inapendelewa au la na sababu zilizochangia hali hii. Katika utafiti huu, tulichukulia kwamba mielekeo chanya kuhusu Kiswahili inaashiria kwamba wahusika wanaipenda lugha hii ilhali mielekeo hasi inaashiria kwamba wahusika hawaipendi. Tulichukulia pia kwamba watu wengi wanapoitumia lugha husika, ina maana kwamba wanaipendelea kuliko lugha zingine. Matokeo ya utafiti kuhusu idadi ya watumiaji wa lugha mbalimbali katika mnada ni yafuatayo:

**Jedwali 4.6: Mielekeo ya wauza mifugo Mmadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi**

| LUGHA | IDADI YA WASAILIWA | ASILIMIA |
|---|---|---|
| Kiswahili | 7 | 20 % |
| Kinandi | 16 | 45.7 % |
| Kuchanganya Lugha | 12 | 34.3 % |
| Jumla | 35 | 100 % |

Utafiti huu ulibaini wazi kuwa kuna mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili kati ya wauzaji mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi. Matokeo ya uchunguzi huu yanadokeza kuwa wasailiwa 7 (asilimia 20%) pekee wa sampuli ya utafiti ya wauza mifugo mnadani ndiyo waliopendelea kutumia Kiswahili katika kuendeleza biashara yao mnadani. Inatokea kwamba katika lugha ya Kinandi, wasailiwa 16 (asilimia 45.7%) wanapendelea lugha hii. Lugha ya Kinandi basi ndiyo lugha inayoonyesha mwelekeo chanya zaidi katika kaunti ya Nandi miongoni mwa

wauza mifugo mnadani kama lugha mwafaka ya kufanyia biashara ikifuatwa na kuchanganya zote ambapo kuna wasailiwa 12 (asilimia 34.3%).

Matokeo haya yanawakilishwa kimchoro kwa kutumia kielelezo cha pai chati kifuatacho:

**Kielelezo 4.1: Mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi**




Mielekeo hii ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi kama lugha ya biashara inalingana na mielekeo na jinsi lugha hizi zinavyotumiwa kijumla kama lugha za kibiashara nchini Kenya. Iraki (2004) anafafanua kwamba lugha za kiasili nchini Kenya, kwa mfano Kinandi, zina wajibu wa kufanikisha mawasiliano ya kibiashara mashinani.

Mielekeo hasi ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili kama lugha mwafaka ya kibiashara mashinani ilisaidia kueleza sababu zinazochangia wauza mifugo mnadani kutopendelea kufanya mazungumzo kwa Kiswahili ambacho ni lugha ya taifa kisha kumilisi lugha hiyo kwa viwango vya chini. Hii inasababisha kuwa na athari hasi kwa maendeleo ya Kiswahili nchini hata kwa vizazi vijavyo.

### 4.3.2 Vipengele vinavyosababisha mielekeo mbalimbali ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kubaini mambo ambayo husababisha mielekeo mbalimbali ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi. Vipengele vilivyotafitiwa ni pamoja na umri wa wauza mifugo mnadani, viwango vya elimu na tofauti za kijinsia za wasailiwa katika Kaunti ya Nandi.

#### 4.3.2.1 Umri wa wasailiwa

Wasailiwa waliulizwa kutaja umri zao. Jedwali lifuatalo la **(4.3)** ambalo lilitajwa pia katika uk. 58, linadhihirisha matokeo ya umri wa wasailiwa. Tunalirudia hapa jedwali hili ili kurahisisha urejeleaji wa data kuhusu umri wa wasailiwa wakati tunapoijadili katika sura hii.

**Jedwali 4.3: Umri wa wasailiwa katika utafiti**

| | UMRI (MIAKA) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **LUGHA** | | **20 – 30** | **31 – 40** | **41 – 50** | **50 na zaidi** | **Jumla** | **Asilimia** |
| | **Kiswahili** | 5 | 1 | 1 | 1 | 8 | 22.9% |
| | **Kiingereza** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Kinandi** | 1 | 3 | 4 | 8 | 16 | 45.7% |
| | **Kuchanganya Zote** | 3 | 5 | 2 | 1 | 11 | 31.4% |

Ni muhimu pia kuiwakilisha hiyo data kimchoro kwa kutumia kielelezo cha bar grafu kifuatacho ili kumpa msomaji picha ya uhusiano kati ya umri wa wasailiwa na matumizi yao ya lugha.

**Kielelezo 4.2 Umri wa wasailiwa katika utafiti**




Kama inavyojitokeza kwenye jedwali hapo juu, asilimia 22.9% ya wasailiwa walipendelea Kiswahili ambapo wale wa kati ya miaka 20-30 walikuwa asilimia

62.5% ikilinganishwa na asilimia 12.5% ya umri kati ya 31-40, 41-50 na 51 na zaidi. Kwa hivyo, wafanyabiashara wa umri mdogo wanapendelea Kiswahili ikilinganishwa na wale wa umri mkubwa.

Kwa upande mwingine, kati ya asilimia 45.7% ya wasailiwa waliopendelea Kinandi, asilimia 50% ni wale wa umri wa miaka 50 na zaidi ikifuatiwa na asilimia 25% ambao wana umri kati ya 41 na 50; wale wa kati ya 31-40 ni asilimia 18.8% na ndio wanaopendelea Kinandi. Wale wa umri kati ya 20 na 30 ni asilimia 6.3% na ndio waliopendelea Kinandi kwa biashara. Kwa hivyo wafanyabiashara wenye umri mkubwa ndio waliopendelea Kinandi kwa biashara.

Wasailiwa waliopendelea kuchanganya lugha zote ni asilimia 31.4% ambapo wengi wao ni wale wa kati ya miaka 31-40. Sababu kuu ni kurahisisha mawasiliano ikikumbukwa kwamba wao wana umilisi wa lugha zaidi ya moja. Matokeo haya yanaoana na matokeo ya utafiti wa Myers-Scotton (1997) aliyesema kuwa kuchanganya lugha inatokana na kupendelea lugha zote azijuazo mtu, na vilevile kwa sababu ya kurahisisha mawasiliano miongoni mwa wanauwingi lugha.

Asilimia 45.5% ya wasailiwa wote waliopendelea kuchanganya lugha walikuwa wa umri kati ya miaka 31 – 40 ikifuatiwa na wale walio na umri wa kati ya miaka 20 – 30 ambao ni asilimia 27.3%. Sababu walizotoa kuhusu lugha

wanayoipendelea kutumia kwa biashara ni kuwa wana umilisi mzuri wa lugha yao ya kwanza na kuwa hawaelewi kanuni za lugha ya Kiswahili. Sababu hizi ziliibuliwa kutokana na swali la 5(b) la hojaji kwa wauza mifugo inayopatikana kwenye **kiambatisho cha 2.** Mtafiti aliweza kuthibitisha ushahidi huu kupitia kwa maoni aliyopata kutoka kwa wasailiwa wakati aliposhirikiana nao moja kwa moja katika shughuli ya kuuza na kununua mifugo. Mbali na hojaji, kushiriki ni mbinu nyingine tuliyotumia kukusanya data kama tulivyoeleza katika sehemu ya **3.2.6.** Kwa hivyo, wanaonelea Kiswahili ni kigumu na kuwa sio lugha yao halisi. Basi hii ikawa dhihirisho ya mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili.

Matokeo kutokana na utafiti yanadhihirisha kuwa mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili kutegemea tofauti zao za kiumri ni chanya na hasi. Wasailiwa wenye umri mkubwa hawapendelei lugha ya Kiswahili kwa vile hawakutagusana na Kiswahili hapo awali. Haya yalithibitishwa na maoni waliyotoa wakati mtafiti aliposhirikiana nao kuuza na kununua mifugo. Kutokana na jedwali letu hapo juu, wengi wa wauza mifugo mnadani wa umri mdogo hupendelea lugha ya Kiswahili. Matokeo haya yanakubaliana na matokeo ya Abdullah, Safrudin, Taib, & Ismail (2018:775) waliosema kuwa watu wa umri mmoja mara nyingi hutumia lugha sawia.

Japo kuna watu wa umri tofautitofauti katika jamii, mtu anaweza kutumia mitindo mbalimbali kwa wazungumzaji wengine. Kwa mtazamo wa utafiti huu basi, wale

wa umri mdogo hupendelea lugha ya Kiswahili ili kujitambulisha na wanarika wenzao mnadani. Wengi wa wale wa umri mkubwa hasa wa kati ya umri wa miaka 50 na zaidi, hutumia lugha ya Kinandi kwa sababu wanaamini kuwa hawaelewi kanuni za Kiswahili, hivyo basi wanachukulia kwamba Kiswahili ni lugha ambayo ni ngumu.

Kwa wafugaji Wanandi, lugha yao sio tu chombo cha mawasiliano, bali ni sehemu muhimu sana ya urithi wao wa kitamaduni na utambulisho wa kijamii. Kama anavyosema Kirilenko (2024: 22), lugha ni kitambulisho cha watu wa jamii inayotumia lugha moja. Watu huonyesha mshikamano wao wakiwa na wenzao kutoka jamii moja, hasa ikiwa lugha wanayotumia ina uhai wa kiwango cha juu katika jamii.

Lugha ya Kinandi inahifadhi maarifa ya kiasili ya Wanandi kuhusu mazingira (kama vile aina za mimea ya kulisha mifugo), aina za wanyama wa kufugwa, bidhaa zinazotokana na mifugo, magonjwa ya mifugo, dalili zake na jinsi ya kuyakinga na kuyatibu, na shughuli za ufugaji kwa jumla, ambavyo ni muhimu kwa maisha yao. Maarifa haya yote ya kiasili huhifadhiwa katika lugha yao. Kwa hivyo, si ajabu kwamba wengi wao, hasa wale walio na umri mkubwa, hupendelea kuitumia lugha yao ya Kinandi katika kuendeleza shughuli za kunadi mifugo. Hii ndio lugha inayowawezesha kujieleza vizuri zaidi kuhusu maarifa hayo kuliko lugha nyingine yoyote.

Utafiti wa Kotut na McCrickard (2022) umethibitisha kwamba wazee wa jamii ya Kalenjin wanachukuliwa kuwa wamiliki wa maarifa ya kiasili, ambapo wanajamii wasiokuwa mtandaoni hutafuta ushauri wao kuhusu matumizi ya maarifa hayo katika maisha yao ya kila siku. Hii ni kwa sababu wana tajriba na ufasaha mkubwa katika utamaduni na lugha yao asili. Hivyo basi, inawezekana kwamba utamaduni na mazingira huathiri pia mielekeo ya lugha ya wauza mifugo mnadani, hasa wazee. Haya yalishuhudiwa pia na mtafiti aliposhirikiana moja kwa moja na wasailiwa hao katika shughuli ya kuuza na kununua mifugo mnadani.

Uelewa wa mielekeo ya wafugaji kuhusu lugha na shughuli zao za ufugaji ni muhimu sana katika kubuni mikakati ya kusaidia kuhifadhi mazingira na kuleta maendeleo katika jamii zao.

#### 4.3.2.2 Uhusiano uliopo kati ya umri na kuchanganya lugha

Uchanganuzi wa data unaonyesha kwamba visa vingi vya kuchanganya lugha wakati wa kunadi mifugo hutokea miongoni mwa wauzaji walio na umri wa kati ya miaka 20 na 40 ambacho ni kipindi cha umri wa vijana. Visa vya wauzaji wazee wa kati ya umri wa miaka 41 na 50 na zaidi kuchanganya lugha ni vichache mno. Hali hii inaweza kufasiriwa kwa njia mbili: kwanza, wauzaji vijana wamepitia katika mfumo wa elimu wa 8-4-4 ambao umewalazimisha kujifunza lugha ya Kiingereza na Kiswahili shuleni hivyo basi wamezoea kubadili msimbo wanapowasiliana. Kwa upande mwingine, wauzaji wazee wengi walisomea katika mfumo wa elimu wa 7-4-2-3 ambao haukuwalazimisha kujifunza Kiswahili

shuleni na hata baadhi ya wazee hawakusoma hadi shule ya upili. Kwa hivyo wengi hawafahamu vizuri lugha ya Kiswahili na Kiingereza ambazo zingewawezesha kuchanganya msimbo.

Fasiri ya pili ni kwamba, wazee kawaida hupendelea zaidi kutumia na kuhifadhi lugha yao asili ambayo huwatambulisha kama jamii ya Wanandi. Si kawaida yao kuchanganya maneno ya lugha yao na maneno ya lugha zingine. Lakini vijana hupenda kujitambulisha kupitia kwa mtindo wao wa uzungumzaji wa kuchanganya lugha. Kwa ambavyo vijana wamekulia katika mazingira ya ulumbi (wingi-lugha) na mijini, baadhi yao hawana umilisi mkubwa wa lugha yao asili na hivyo basi hawawezi kujieleza kwa ufasaha kwa Kinandi. Kwa hivyo wao hufidia upungufu huo wa kiisimu kwa kuchanganya Kinandi, Kiingereza na Kiswahili. Kwa mujibu wa Myers-Scotton (1993) akinukuliwa na Githinji (2014:46), matumizi ya mbinu hii ya kuchanganya ndimi na kubadili msimbo huwawezesha Wakenya kujitwalia "...manufaa yanayotokana na hadhi ya lugha ya Kiingereza na vilevile kujitambulisha kama Wakenya kwa kutumia Kiswahili huku wakizipa lugha zao za kiasili nafasi katika mawasiliano yao."

Utafiti ulidhihirisha pia kwamba wale wauzaji mifugo waliokuwa wanabadili msimbo walikuwa wanafanya hivyo wakizingatia muktadha wa mawasiliano. Kwa kawaida, muktadha wa kupiga mnada mifugo unajumuisha wateja wa kutoka jamii mbalimbali kama ilivyo kawaida ya mahali popote palipo na soko. Kwa hivyo ni

kawaida lugha ya Kiswahili kutumiwa ili kuwasiliana na wateja wa kutoka jamii mbalimbali kwa sababu wauzaji Wanandi wanachukulia kwamba wateja hao “wageni’ hawafahamu lugha ya Kinandi.

Lakini pindi muuzaji anapogundua kwamba mnunuzi mtarajiwa anatoka jamii ya Wanandi, basi papo hapo muuzaji hubadili msimbo na kuanza kuzungumza na mteja huyo Kinandi kama ishara ya kujitambulisha naye kama “’ndugu wa kutoka jamii moja.” Lakini mteja mwingine “mgeni” anapokuja kuulizia bei ya mfugo, basi muuzaji anaweza tena kubadili msimbo na kurejelea Kiswahili anapoanza kuzungumza na mgeni huyo wa pili. Kwa hivyo msimbo wa Kiswahili unaweza kutumiwa pale ambapo muuzaji anataka kuwasiliana na wateja “wageni” wasiotoka jamii ya Kinandi, ilhali msimbo wa Kinandi unatumiwa wakati wa kuwasiliana na wateja wanaofahamu Kinandi. Mtafiti alithibitisha matumizi haya ya lugha alipokuwa akishirikiana na wasailiwa kunadi mifugo.

Lakini hata pale ambapo msimbo wa Kiswahili hutumiwa wakati wa kuwasiliana na wateja “wageni”, mara kwa mara muuzaji anaweza kusikika akichopeka baadhi ya maneno ya Kinandi katika sentensi zake za Kiswahili hasa pale ambapo amepungukiwa na msamiati wa Kiswahili wa kutajia vitu fulani vinavyohusiana na mifugo. Kauli hii inaungwa mkono na Bhatia (2008) ambaye anasema kwamba wakati mwingine watu huchanganya maneno ya lugha zao za kwanza katika mazungumzo ili kuepuka hali ya ujumbe kutoeleweka iwapo watatumia lugha

nyingine. Ohia (2023) vilevile anaongezea kwamba kizazi kichanga cha jamii ya Wa-Ogba kinachozungumza Kiingereza kama lugha ya pili huingiza maneno ya Ki-Ogba katika mazungumzo yao ili kuficha upungufu wao wa umilisi wa Kiingereza.

Tabia hii ya kuchanganya lugha miongoni mwa wauza mifugo inafanana na kisa kinachotokana na utafiti aliofanya Myers-Scotton mjini Nairobi kuhusu mgeni anayetembelea kampuni moja ambapo mlinzi wa hiyo kampuni anaanza kwa kuzungumza naye kwa Kiswahili (lugha ya kuzungumza na wageni au wateja kazini). Lakini mlinzi huyo anapogundua kwamba mgeni huyo anatoka katika jamii yake ya Waluyia kutoka Magharibi ya Kenya, anabadili msimbo na kuanza kuzungumza naye lugha ya jamii yao Kiluyia ili kujitambulisha naye kama "ndugu wa kutoka jamii moja" badala ya kuonekana kama watu wasiojuana. Lakini mgeni mwingine anapokaribia, mlinzi huyo anabadili tena msimbo na kuanza kuzungumza naye Kiswahili (Mesthrie, et.al, 2000:167-168).

Kwa ujumla, inaonekana kwamba wauzaji mifugo walikuwa wanachanganya lugha kwa sababu mbalimbali kama vile: kupendelea lugha zote azijuazo mtu, kurahisisha mawasiliano, kupungukiwa na msamiati wa lugha hizo, kuashiria hasira au maudhiko ya mzungumzaji, kuashiria hali ya mzungumzaji kuwa na maarifa mengi, hali ya kutafuta uhusiano mwafaka na mnunuzi mtarajiwa, njia ya kuashiria mabadiliko katika mada ya mazungumzo, kujitambulisha na

wazungumzaji wa lugha fulani na hata wakati mwingine kuwatenga wazungumzaji wa lugha fulani kimawasiliano. Hata hivyo, sababu kamili ya kubadili na kuchanganya lugha miongoni mwa wauzaji mifugo wa Kinandi inaweza tu kufasiriwa kwa kuzingatia muktadha mahsusi wa mazungumzo.

#### 4.3.2.3 Viwango vya elimu

Elimu pia inaweza kuathiri mielekeo ya wafugaji kuhusu matumizi ya lugha. Ingawa baadhi ya wafugaji wanaweza kupendelea kutumia lugha ya taifa, ambayo watu wengi huona kwamba inafaa zaidi kufanikisha shughuli za kibiashara, wengine huenda wakaipa kipaumbele lugha yao asili ya Kinandi kwa sababu za kitamaduni. Kiwango cha elimu alichofikia mfugaji kinaweza kuathiri aina ya lugha atakayochagua kutumia katika kunadi mifugo, kama ni Kinandi, Kiswahili au Kiingereza. Vile vile, kiwango cha elimu cha mnunuzi na lugha anazofahamu kitaamua ni lugha ipi ambayo itatumiwa na wahusika (muuzaji na mnunuzi) katika kunadi mifugo. Wanaweza kutumia lugha moja au zaidi kwa kubadili na kuchanganya msimbo ili kufanikisha mawasiliano.

Lugha ya Kiswahili imepatiwa umuhimu mkubwa kwenye elimu nchini Kenya. Kiswahili ni lugha ya taifa ambayo inawakilisha watu wanaotoka makabila tofauti, kisiasa, kitamaduni na kijamii (Mathooko, 2007). Katika kaunti ya Nandi, lugha hii ya taifa inasusiwa na wengi na kupitia kwa utafiti uliofanywa, wengi wa wakaazi wa eneo hili wana mielekeo hasi kukihusu Kiswahili kupitia kwa lugha inayotumiwa minadani. Walio na viwango vya chini vya elimu (shule ya msingi)

walidhihirisha mielekeo hasi kwa Kiswahili. Kulingana na wao, Kiswahili kinafaa kutumiwa kwenye shughuli nyingine za kijamii kama shuleni, ofisini na kazini na wala sio mnadani.

Mielekeo ya wasailiwa wenye viwango vya juu vya elimu kuhusu Kiswahili ilikuwa chanya ambapo walikubaliana na hoja inayosema kwamba, Kiswahili ni lugha ya taifa na iliyo na dhima ya kuwaleta pamoja watu kutoka jamii tofauti. Aidha, walipendelea matumizi ya Kiingereza kwa sababu ya hali ya mabadiliko yanayofanyika ulimwenguni kwa jumla kila uchao. Inavyojitokeza ni kuwa elimu humfanya mtu kupenda uwililugha na kuwa mwanawingilugha. Hali hii imedhihirika ambapo walio na elimu ya chini wanaonekana kuwa na mielekeo isiyopendelea lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na wale ambao wana elimu ya juu walio na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili.

Kwa kuangazia viwango vya elimu, wauza mifugo mnadani wana viwango tofauti vya elimu ambapo kuna mmoja aliyesoma hadi chuo kikuu, kuna wengine waliofika vyuo anuai na vilevile kuna wale waliomalizia shule za msingi na wale ambao kiwango chao cha elimu ni sekondari. Matokeo ya mielekeo yao ni ifuatavyo:

**Jedwali 4.7: Viwango vya elimu vya wasailiwa**

| | **Shule ya Msingi** | **Asilimia** | **Shule ya Upili** | **Asilimia** | **Vyuo Anuai** | **Asilimia** | **Vyuo Vikuu** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | 2 | 15.4 | 3 | 21.4 | 1 | 14.3 | 1 | 100 |
| **Kinandi** | 8 | 61.5 | 7 | 50 | 3 | 42.9 | 0 | 0 |
| **Kiingereza** | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 14.3 | 0 | 0 |
| **Kuchanganya zote** | 3 | 23.1 | 4 | 28.6 | 2 | 28.6 | 0 | 0 |
| **Jumla** | 13 | 100 | 14 | 100 | 7 | 100 | 1 | **100** |
| **Asilimia** | 37.1 | | 40 | | 20 | | 2.9 | **100** |

Kutokana na jedwali hili, wauza mifugo wengi wamesoma hadi kiwango cha shule ya upili. Mfumo wa elimu nchini Kenya unahitaji Kiswahili kifunzwe na kitahiniwe na hata kitumiwe katika kufunza, hali inayowapa wahusika mwono kinyume na wazee wanaoshikilia Kinandi. Si ajabu kuwa mwelekeo wao ni hasi.

Matokeo haya yanaweza kuwakilishwa kimchoro kwa kutumia kielelezo cha bar grafu kifuatacho:

**Kielelezo 4.3: Viwango vya elimu vya wasailiwa**




Kutokana na matokeo kwenye jedwali kuhusu viwango vya elimu, ilidhihirika wazi kuwa viwango vya elimu huathiri jinsi watu wanavyoweza kupendelea au kutopendelea lugha moja kwa nyingine. Kutokana na utafiti huu, asilimia 100% ya waliosoma hadi kiwango cha juu cha elimu hawana tatizo kutumia Kiswahili kunadi mifugo mnadani. Kuhusu wasailiwa waliosoma hadi viwango vya vyuo anuai, asilimia 14.3% wanapendelea kutumia Kiswahili na Kiingereza, asilimia 28.6% wanapenda kuchanganya lugha zote, na asilimia 42.9% wanapenda kutumia lugha ya Kinandi kunadi mifugo. Hii inadhihirisha ya kwamba wafanyibiashara waliosoma hadi vyuo anuai wanapendelea Kinandi katika shughuli zao za kibiashara.

Wasailiwa waliosoma hadi kiwango cha shule ya upili na wanapendelea lugha ya Kiswahili ni asilimia 21.4%, wale wa kuchanganya lugha ni asilimia 28.8% na wanaopendelea lugha ya Kinandi ni asilimia 50%. Wasailiwa walio na kiwango cha elimu cha shule ya msingi na wanaopendelea Kiswahili ni asilimia 15.4%, wale wanaochanganya lugha ni asilimia 23.1%, wale wanaopendelea Kinandi ni asilimia 61.5%. Kutokana na matokeo hayo ya utafiti, inadhihirika kwamba lugha inayopendelewa kunadi mifugo mnadani katika Kaunti ya Nandi ni Kinandi, kwa hivyo mielekeo ya wauza mifugo katika kaunti ya Nandi kuhusu Kiswahili ni hasi.

Sababu kuu ya kushikilia lugha ya Kinandi ni utamaduni uliofungamanishwa na mifugo ikikumbukwa kuwa lugha ni kitambulisho cha jamii na hivyo wauza mifugo hupenda kujitambulisha na utamaduni wake. Vilevile hali hii husababishwa na Wanandi kuwa na imani kuwa hawana uelewa mzuri kwa lugha ya Kiswahili, na hivyo kutaka kurahisisha mawasiliano wakitumia lugha wanayoielewa vizuri nayo ni lugha ya Kinandi.

#### 4.3.2.4 Jinsia

Uchunguzi huu ulizingatia sana kigezo cha jinsia ya wasailiwa ili kuhakikisha kwamba kulikuwa na ushirika unaolingana wa wahojiwa kijinsia katika sekta ya biashara. Mtafiti alitumia kifaa cha Lickert ili kumsaidia kutofautisha hisia chanya na hisia hasi za wahusika wa jinsia ya kike na ya kiume. Jedwali lifuatalo lilidhihirisha matokeo ya utafiti kuhusu suala la jinsia.

**Jedwali 4.8: Matokeo ya mielekeo kijinsia**

| Jinsia | Idadi | Asilimia % | Hisia Chanya | Asilimia % | Hisia Hasi | Asilimia % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kiume** | 28 | 80 | 18 | 75 | 10 | 90.9 |
| **Kike** | 7 | 20 | 6 | 25 | 1 | 0.1 |
| **Jumla** | 35 | 100 | 24 | 100 | 11 | 100 |

Matokeo haya yanaweza kuwakilishwa kimchoro kwa kutumia kielelezo cha bar grafu kifuatacho:

**Kielelezo 4.4: Matokeo ya mielekeo kijinsia**




Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa asilimia 80% ya wauza mifugo mnadani walikuwa wanaume na asilimia 20% walikuwa wanawake. Hii inadhihirisha kuwa wengi wa wasailiwa wanaouza mifugo mnadani ni wanaume. Wanawake

waliopendelea kutumia Kiswahili kunadi mifugo mnadani ni asilimia 85.7% na wanaume walikuwa asilimia 64.3%. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa wanawake wengi wana mielekeo chanya kwa Kiswahili ikilinganishwa na wanaume. Ni muhimu kujadili sababu zinazowapelekea wanawake kupendelea Kiswahili zaidi ya wanaume.

Kuhusu athari ya jinsia kwa mielekeo kuhusu lugha, ipo mitazamo miwili kinzani inayoshikiliwa na wanaelimu-lahaja wa kijamii (Shazu, 2014). Kwanza, kuna mtazamo unaodai kwamba wanawake hupendelea kutumia lugha ya hadhi ya juu kuliko wanaume kwani wao hujali sana jinsi wanavyoonekana mbele ya watu. Hivyo basi aina ya lugha na maumbo ya lugha sanifu wanayotumia katika mawasiliano huakisi hadhi ya juu wanayotaka kujinasibisha nayo. Jambo hili limewahi kuthibitishwa, kwa mfano, na Labov (1966) katika utafiti wa New York City, Trudgill (1983) katika utafiti wake wa Norwich, Uingereza, na Mesthrie (2000:222).

Kwa upande mwingine, kuna mtazamo wa pili unaopendekezwa na mwanaisimu wa Kimarekani, Lakoff (1975), ambao unashikilia kwamba wanawake hutumia lugha inayoimarisha hadhi ya chini waliyo nayo katika jamii. Hii ina maana kwamba wanawake wanapenda kutumia lugha inayochangia kuwadunisha zaidi. Kwa maneno ya Lakoff akinukuliwa na Shazu (keshatajwa), wanawake "wanakula njama kushiriki katika kudunishwa kwao" kupitia kwa uzungumzaji wao (uk. 93).

Lakoff (keshatajwa) ametambua sifa nyingi za kimatamshi, kisarufi na kiisimu-jamii zinazobainika zaidi katika usemi wa wanawake kuliko usemi wa wanaume. Baadhi ya sifa hizo ni kama vile matumizi ya: maumbo ya sarufi sanifu; vivumishi visivyo na maana dhahiri k.v. ajabu, tamu, zuri; kiimbo cha kupanda kwenye kauli; vitambulisho vya maswali k.v. sivyo? sindiyo?; vijalizo vya usemi k.v. naam, yaani, eeh, n.k.; unyenyekevu; kutodakia au kutoingilia mazungumzo; na kuendesha mazungumzo kwa ushirikiano zaidi kuliko ushindani.

Kwa maoni yetu, mtazamo wa kwanza unaodai kuwa wanawake hupenda kutumia lugha inayowanasibisha na hadhi ya juu unaelekea kuwa na ushawishi zaidi katika muktadha wa wanawake wa Kinandi wanaonadi mifugo. Sio katika matumizi ya lugha tu bali hata katika mitindo ya mavazi, ni wazi kwamba wanawake wanapenda sana kutumia mitindo mipya kuliko wanaume kwani wanajali sana mwonekano wao hadharani. Kiswahili kina hadhi ya juu kuliko Kinandi kwa sababu ni lugha ya taifa na pia lugha rasmi nchini Kenya. Hivyo basi, huenda ikawa wanawake wa Kinandi wanapokitumia, wanahisi kwamba kinachangia kuinua hadhi yao katika jamii hasa ikizingatiwa kwamba aghalabu jamii nyingi huwapa wanaume hadhi ya juu kuliko wanawake.

Watafiti wengi (kwa mfano, Brown, 1980; Holmes, 1995; Coates, 2013; & Shazu, 2014) wanashikilia kwamba wanawake wengi hutumia lugha ya unyenyekevu kuliko wanaume kulingana na matarajio ya jamii ambamo wamelelewa. Bado

hatuna uhakika iwapo uchaguzi kati ya matumizi ya Kinandi na Kiswahili miongoni mwa wanawake unahusiana na hoja hii au la. Hata hivyo, tunakisia kwamba huenda ikawa wanawake wa Kinandi hujihisi wanyeyekevu zaidi wanapotumia Kiswahili kunadi mifugo kuliko wanapotumia lugha yao asili ya Kinandi na hiyo huenda ikawa ndiyo sababu inayowafanya wapendelee kutumia Kiswahili kuliko wanaume. Katika sajili ya kibiashara, unyenyekevu wa muuzaji ni sifa muhimu sana katika kumshawishi mteja kununua bidhaa.

Watafiti wa ubongo wamedai kwamba wanawake wana uwezo mkubwa wa kuzungumza lugha kuliko wanaume kwa sababu wao hutumia upande wa kushoto na wa kulia wa ubongo kushughulikia lugha ilhali wanaume hutumia upande wa kushoto pekee (Ringle, 2024). Madai haya yanaweza kuwa na ukweli hasa tukizingatia kwamba wanafunzi wengi wa kike hufanya vizuri katika mitihani ya masomo ya lugha kuliko wenzao wa kiume. Ukweli huu wa kibayolojia huenda ikawa unachangia wanawake wengi wa Kinandi kufurahia, kujifunza na kutumia Kiswahili zaidi katika kunadi mifugo kuliko wanaume. Huku wanaume wanapong’ang’ana na kujieleza kwa Kiswahili, wanawake wanaweza kujieleza kwa urahisi zaidi kwa sababu ya uwezo wa lugha waliozaliwa nao.

### 4.3.3 Athari za mielekeo ya lugha kwa maendeleo ya Kiswahili katika jamii

Utafiti huu ulidhamiria kubainisha jinsi mielekeo mbalimbali ya wauza mifugo mnadani kuhusu lugha inavyoathiri maendeleo ya Kiswahili katika jamii. Mtafiti aliandaa hojaji iliyokuwa na kauli kumi na kuwapa wasailiwa ili watoe maoni yao

kuhusu kauli hizo. Mielekeo yao ilibainishwa kupitia kwa mwitiko wao kuhusu kauli kumi zifuatazo. Hivyo basi sehemu hii inawasilisha matokeo yanayohusu mwitiko wa wasailiwa kuhusu kauli hizo:

a) Naipenda lugha ya Kiswahili

b) Lugha ya Kiswahili ina manufaa katika maisha kwa ujumla

c) Naridhishwa na nafasi ya Kiswahili nchini.

d) Lugha ya Kiswahili hutumika katika shughuli mbalimbali za kijamii wakati wowote.

e) Kiswahili ni kigumu mno.

f) Natumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na wenzangu mnadani.

g) Lugha ya Kiswahili ina manufaa kwangu kama Mkenya.

h) Siridhishwi na jinsi Kiswahili kilivyofunzwa shuleni.

i) Lugha ya Kiswahili inastahili kutumika katika mawasiliano yetu ya kila siku.

j) Ujuzi wa lugha hii ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa hutegemea mazingira alimokulia mzungumzaji.

Jedwali lifuatalo linaonyesha mwitiko wa wasailiwa kuhusu kauli hizo:

**Jedwali 4.9: Athari za mielekeo ya lugha kwa maendeleo ya Kiswahili katika jamii**

| | Maswali | Idadi | Alama ya chini | Alama ya juu | Wastani | Mwachano |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Naipenda lugha ya Kiswahili | 35 | 2.00 | 4.00 | 3.3750 | .74402 |
| 2. | Lugha ya Kiswahili ina manufaa katika maisha kwa ujumla | 35 | 3.00 | 4.00 | 3.5000 | .53452 |
| 3. | Naridhishwa na nafasi ya Kiswahili nchini. | 35 | 3.00 | 4.00 | 3.6250 | .51755 |
| 4. | Lugha ya Kiswahili hutumika katika shughuli mbalimbali za kijamii wakati wowote. | 35 | 3.00 | 4.00 | 3.7500 | .46291 |
| 5. | Kiswahili ni kigumu mno. | 35 | 3.00 | 4.00 | 3.7500 | .46291 |
| 6. | Natumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na wenzangu mnadani. | 35 | 3.00 | 4.00 | 3.8750 | .35355 |
| 7. | Lugha ya Kiswahili ina manufaa kwangu kama Mkenya. | 35 | 3.00 | 4.00 | 3.8750 | .35355 |
| 8. | Siridhishwi na jinsi Kiswahili kilivyofunzwa shuleni. | 35 | 3.00 | 4.00 | 3.8750 | .35355 |
| 9. | Lugha ya Kiswahili inastahili kutumika katika mawasiliano yetu ya kila siku. | 35 | 4.00 | 4.00 | 4.0000 | .00000 |
| 10. | Ujuzi wa lugha hii ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa hutegemea mazingira alimokulia mzungumzaji. | 35 | 3.00 | 4.00 | 3.7850 | .34550 |
| | Valid N (Listwise) | 35 | | | | |

Kutokana na utafiti huu kuhusu athari za mielekeo ya hizo lugha kwa maendeleo ya Kiswahili, jedwali la (**4.9**) hapo juu linaonyesha mwitiko wa wasailiwa kuhusu kauli hizo. Matokeo yalionyesha alama za wastani zifuatazo kuanzia kauli ya kwanza hadi ya kumi: 3.3750, 3.5000, 3.6250, 3.7500, 3.7500, 3.8750, 3.8750, 3.8750, 4.0000 na 3.7850 mtawalia. Matokeo haya yanaoana na mawazo ya Holmes (2013) aliyechunguza namna watu wanavyotumia lugha katika shughuli mbalimbali katika jamii iliyo na wingi lugha. Anasema kuwa wanajamii katika shughuli zao za kawaida hutoa habari muhimu kuhusu matumizi ya lugha na namna ambavyo watu wanatumia lugha kama njia ya kujitambulisha.

Mielekeo hasi ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili iliathiriwa na masuala ya kijamii. Wasailiwa wengi walipendelea matumizi ya lugha ya mama ili waweze kujitambulisha kijamii. Wasailiwa wengi walieleza kuwa ni kupitia matumizi ya lugha ya kiasili ya Kinandi ambapo utamaduni wa jamii hiyo hupokezwa kwa vizazi mbalimbali. Aidha, kutokana na maelezo ya wasailiwa, matumizi ya lugha ya kiasili ya Kinandi ni nyenzo muhimu katika kurahisisha mawasiliano baina ya wanajamii na kukuza utangamano.

Mielekeo hasi ya wauza mifugo mnadani inaathiri matumizi ya Kiswahili katika jamii. Hii ni kwa sababu mielekeo hiyo inatatiza juhudi za kutumia Kiswahili kama chombo cha kujenga umoja na utangamano wa Wakenya wanaoishi kaunti ya Nandi na wanaotoka jamii mbalimbali ambao wangependa kukutana na

kutumia Kiswahili kama lugha ya kuwaunganisha kibiashara. Hali hii inaweza kuathiri vibaya uchumi wa kaunti ya Nandi na nchi ya Kenya kwa jumla.

Kwa upande mwingine, mielekeo chanya ya baadhi ya wauza mifugo katika kaunti ya Nandi inasaidia pakubwa kuimarisha Kiswahili kama lugha rasmi ya kutolea huduma mbalimbali katika kaunti ya Nandi na pia kama lugha ya taifa. Wauza mifugo wanapofurahia kutumia Kiswahili katika biashara, basi wanaweza kufurahia pia kupokea huduma mbalimbali zinazotolewa na kaunti kupitia lugha hiyo. Hali hii itasaidia sana kutekeleza Kiswahili kama lugha rasmi katika serikali za magatuzi kuambatana na *Katiba ya Kenya* (2010).

Tofauti za mielekeo kuhusu Kiswahili na Kinandi kwa kuzingatia vigeu vya jinsia, umri, na elimu, zinaweza pia kuathiri maendeleo ya Kiswahili katika kaunti ya Nandi. Kuhusu athari ya umri kwa mielekeo, matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kwamba wafanyabiashara wa umri mdogo (kati ya miaka 20 na 30) wanapendelea zaidi kutumia Kiswahili kuliko wale wa umri mkubwa ilihali wafanyabiashara wa umri mkubwa wanapendelea Kinandi. Kwa hivyo, tunaweza kubashiri kwamba matumizi ya Kiswahili katika jamii ya Nandi yataongezeka katika miaka ijayo kwa sababu ya vijana kuichangamkia lugha hii.

Kuhusu athari ya kiwango cha elimu kwa mielekeo, utafiti huu umeonesha kwamba wafanyabiashara walio na viwango vya chini vya elimu (kwa mfano, shule ya msingi) hawapendelei sana Kiswahili wakilinganishwa na wenzao walio na elimu ya kiwango cha juu ambao wanapendelea Kiswahili na Kiingereza. Hivyo basi, tunaweza kubashiri kwamba, iwapo watu wengi wataendelea kupata elimu ya juu katika kaunti ya Nandi, basi kuna matumaini ya Kiswahili kuendelea zaidi siku za usoni.

Kuhusu athari ya jinsia kwa mielekeo, matokeo ya utafiti huu yamethibitisha kwamba wanawake wengi wanapendelea kutumia Kiswahili wakilinganishwa na wanaume. Ingawa idadi ya wanawake waliosailiwa ilikuwa ndogo, matokeo haya yanatuelekeza kubashiri kwamba wanawake wengi wakishirikishwa katika shughuli za biashara, basi Kiswahili kitaendelea zaidi katika kaunti ya Nandi.

## 4.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumewasilisha, tukachanganua na kujadili data kutoka kwa utafiti huu ili kudhihirisha mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu lugha ya Kiswahili. Sura hii imetimiza malengo matatu ya utafiti huu ambayo ni: kupambanua mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kwa lugha ya Kiswahili katika kaunti ya Nandi; kubainisha mambo ambayo husababisha mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu lugha ya Kiswahili; na kuchunguza athari ya mielekeo hiyo ya lugha kwa

maendeleo ya Kiswahili katika jamii hii. Kutokana na utafiti huu, imebainika kwamba wauza mifugo mnadani wana mielekeo mibaya kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa nchini. Wanapendelea lugha ya Kinandi kwa kuwa ni lugha yao asilia na hivyo ni lugha wanayoifahamu vizuri. Vilevile, wanaonelea kuwa lugha ya Kinandi inarahisisha biashara yao.

Takwimu tulizozipata zimetupa picha halisi ya mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi. Vigezo tulivyotumia kubaini mielekeo ni pamoja na lugha, umri wa wasailiwa, jinsia, na kiwango cha elimu. Matokeo yalibaini kuwa mielekeo ya wauza mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi ni hasi na chanya kutegemea umri, kiwango cha elimu na jinsia. Mtafiti ametoa kauli kuhusu data zilizochanganuliwa pamoja na kuziunga mkono kwa kurejelea maoni ya wasomi mbalimbali. Uchanganuzi wa data hizo pia umefanywa kwa kurejelea misingi ya nadharia ya utendaji razini iliyoteuliwa kuongoza utafiti huu. Hivyo basi, sura ifuatayo inalenga kuhitimisha utafiti huu kwa kutoa muhtasari wa matokeo yaliyopatikana.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura zilizotangulia zimeshughulikia vipengele mbalimbali vinavyohusu mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi. Sura hii ya tano ndiyo inahitimisha utafiti kwa kutoa muhtasari wa tasnifu nzima, matokeo ya utafiti na umuhimu wake, changamoto zilizomkumba mtafiti na pia mapendekezo kuhusu utafiti wa baadaye. Mapendekezo yaliyotolewa yanaweza kutegemewa na washikadau katika sekta ya elimu wanapobuni sera na mikakati ya kuimarisha matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wananchi katika sekta mbalimbali za kijamii.

## 5.2 Muhtasari wa utafiti

Madhumuni ya uchunguzi huu yalikuwa ni kueleza namna mielekeo inavyoathiri matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wauzaji mifugo katika minada ya kaunti ya Nandi. Kwa jumla, malengo ya utafiti huu yalikuwa ni: kupambanua mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi. Pili, ni kubainisha mambo ambayo husababisha mielekeo tofautitofauti kuhusu lugha ya Kiswahili miongoni mwa wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi. Mwisho, ni kuchunguza athari za mielekeo hiyo ya lugha kwa maendeleo ya Kiswahili katika jamii ya Wanandi.

Utafiti huu umefanywa katika sura tano. Sura ya kwanza imetoa utangulizi wa utafiti mzima. Sura hii imeshughulikia mambo kama vile: usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti.

Sura ya pili imejadili mapitio ya maandishi ili kubaini pengo la utafiti na kueleza iwapo mielekeo ya hapo awali inaweza kuathiri mielekeo kuhusu lugha nchini kwa sasa. Sura hiyo pia imefafanua misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti huu.

Katika sura ya tatu, mbinu za utafiti zimefafanuliwa na katika sura ya nne, data zilizokusanywa zimewasilishwa, zikachanganuliwa na kujadiliwa ili kujibu maswali na kutimiza malengo ya utafiti. Data zilizokusanywa na kuchanganuliwa zilitokana na minada ya mifugo pekee kwenye masoko ya Lemook, Kabiyet, Chepterit, Maraba, Kibwareng', Kaptumo na Chebarus ambayo yanapatikana katika kaunti ya Nandi. Uchanganuzi wa mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili umefanywa kwa kuongozwa na Nadharia ya Utendaji Razini na kwa kuzingatia nafasi ya Kiswahili kama lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya.

Sababu za mielekeo ya wauzaji wa mifugo mnadani kuhusu matumizi ya Kiswahili zimejadiliwa kwa kurejelea vigeu kama umri wa wasailiwa, viwango vyao vya elimu na jinsia. Vilevile, athari ya sababu hizi kwa mielekeo ya wauza

mifugo zimejadiliwa na matokeo yakawasilishwa kwa kutumia maelezo, majedwali na vielelezo vya pai chati na bar grafu.

Sura hii ya tano inatoa muhtasari wa matokeo muhimu ya utafiti, kueleza changamoto zilizomkumba mtafiti na pia kupendekeza mada za kufanyiwa utafiti zaidi.

## 5.3 Matokeo ya utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanaoana na malengo yetu matatu ya utafiti ambayo ni kupambanua mielekeo ya wauzaji wa mifugo mnadani ambao huzungumza Kinandi kuhusu lugha ya Kiswahili katika kaunti ya Nandi; kubainisha mambo ambayo husababisha mielekeo tofautitofauti kuhusu lugha ya Kiswahili miongoni mwa wauza mifugo mnadani wanozungumza Kinandi; na kuchunguza athari za mielekeo hiyo ya lugha kwa maendeleo ya Kiswahili katika jamii ya wazungumzaji wa Kinandi.

### 5.3.1 Mielekeo ya wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi kuhusu Kiswahili katika kaunti ya Nandi

Kutokana na utafiti huu, ilibainika kuwa wauza mifugo mnadani wanashikilia mielekeo mibaya kuhusu lugha ya Kiswahili inapotumiwa kama lugha ya kufanyia biashara mashinani. Utafiti ulibainisha sababu zinazowafanya wauza mifugo mnadani kutopendelea kuzungumza Kiswahili ambacho ni lugha ya taifa na kisha

kuwapelekea kuwa na viwango vya chini vya umilisi wa Kiswahili nchini hata kwa vizazi vijavyo.

### 5.3.2 Mambo ambayo husababisha mielekeo tofautitofauti kuhusu lugha ya Kiswahili miongoni mwa wauza mifugo mnadani wanaozungumza Kinandi

Kutokana na matokeo ya utafiti kuhusu viwango vya elimu, ilidhihirika wazi kuwa viwango vya elimu huathiri jinsi watu wanavyoipendelea lugha moja kuliko nyingine. Wale waliosoma hadi viwango vya juu vya elimu hawana tatizo kubwa kwa kutumia Kiswahili. Hii inadhihirika pale ambapo asilimia 40% ya walioenda shule ya upili wanapendelea Kiswahili.

Aidha, matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa mielekeo ya wauza mifugo mnadani kuhusu Kiswahili kutokana na tofauti za kiumri ni chanya na hasi. Walio na umri mkubwa hawapendelei kabisa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu hawakukumbana sana na matumizi ya Kiswahili. Kwa mtazamo wa utafiti huu basi, wale wa umri mdogo hupendelea Kiswahili ili kujitambulisha na wanarika wenzao. Wengi hutumia lugha ya Kinandi katika umri mkubwa haswa katika umri wa miaka kati ya 50 na zaidi.

Matokeo ya utafiti pia yalionyesha kuwa wanawake waliopendelea kutumia Kiswahili kunadi mifugo mnadani ni asilimia 87.7% na wanaume walikuwa

asilimia 64.3%. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa wanawake wengi wana mielekeo chanya kuhusu Kiswahili ikilinganishwa na wanaume.

### 5.3.3 Mielekeo ya lugha na athari zake kwa maendeleo ya Kiswahili

Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa mazingira ya mtu yanaweza kumfanya kuwa na mwelekeo chanya au hasi kuhusu Kiswahili. Wengi wa wasailiwa walipendelea kutumia lugha ya mama mashinani kama utambulisho wa jamii yao. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa wengi wa wasailiwa wanauona utambulisho wa aina hii kama njia ya kupokeza utamaduni wa jamii yao kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Vilevile, lugha ya kiasili ilielezewa kama ya kurahisisha mawasiliano baina ya wanabiashara sokoni na kukuza utangamano baina ya wanajamii lugha.

Matokeo ya utafiti huu yameonesha kwamba mielekeo hasi inatatiza juhudi za kutumia Kiswahili kama chombo cha kujenga umoja na utangamano kati ya Wanandi na Wakenya wengine; nayo mielekeo chanya ya baadhi ya wauza mifugo katika kaunti ya Nandi inasaidia pakubwa kuimarisha Kiswahili kama lugha rasmi ya kutolea huduma mbalimbali katika kaunti ya Nandi. Kutokana na athari ya umri, jinsia na kiwango cha elimu kwa mielekeo ya wauzamifugo Wanandi, inaelekea kwamba matumizi ya Kiswahili katika jamii ya Nandi yataongezeka katika miaka ijayo. Hii ni kwa sababu lugha hii inapendelewa zaidi na vijana waliopata elimu ya juu pamoja na wanawake.

## 5.4 Changamoto za utafiti

Mtafiti alipokuwa akifanya utafiti huu, alikumbwa na changamoto nyingi. Kwanza, utafiti huu ulianza kufanywa wakati wa maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19 mnamo mwaka 2020. Hali hiyo ilisababisha mikusanyiko ya watu wa kuuza mifugo mnadani kupigwa marufuku na ikawa vigumu mtafiti kukusanya data katika kipindi hicho. Ilibidi mtafiti asubiri kipindi hicho cha marufuku kiishe ndipo aendeleze utafiti wake. Hali hiyo ilichangia utafiti huu kuchelewa kukamilika.

Pili, baadhi ya wasailiwa walishikilia mielekeo ya kutopendelea lugha ya Kiswahili, hivyo basi hawakutaka mtafiti awahoji kwa Kiswahili wala kuwapa hojaji za Kiswahili kumjazia. Ilibidi mtafiti awabembeleze kushirikiana naye huku akiwahakikishia kwamba matokeo ya utafiti huu yangewafaidi watu wengi hivyo basi kushiriki kwao kulikuwa muhimu sana.

Tatu, mtafiti alikumbwa na shida ya uhaba wa fedha za kugharamia shughuli mbalimbali za utafiti huu. Shughuli hizo ni pamoja na usafiri kwa magari kwenda nyanjani, kupiga simu, kuzuru maktaba mbalimbali, kununua data ili kutumia mtandao na kutolesha nakala za hojaji na sura za tasnifu. Hali hiyo ilimfanya mtafiti kuahirisha shughuli zingine hadi wakati atakapopata pesa za kumwezesha kutekeleza shughuli hizo. Changamoto hii pia ilichangia utafiti kuchelewa kukamilika.

Nne, mtafiti pia aligharamika sana kununua vitabu muhimu vilivyohitajika kwa sababu si vyote vilipatikana maktabani na mtandaoni. Ilibidi pia mtafiti atoe pesa nyingi kutolesha nakala za baadhi ya makala muhimu kutoka katika vitabu muhimu na majarida ambayo hayapatikani mtandaoni.

Tano, kulikuwa na changamoto ya hali ya anga na barabara. Wakati mtafiti alikuwa akikusanya data msimu wa mvua, baadhi ya barabara za wilaya ya Nandi zilikuwa mbaya kiasi cha kutopitika. Kwa hivyo, mtafiti alipata changamoto ya kuwafikia mapema wahojiwa katika minada ya kuuza mifugo.

Sita, mtafiti alikumbana pia na changamoto ya kutafsiri kwa Kiswahili mawazo yaliyomo katika Nadharia ya Utendaji Razini na Nadharia ya Tabia Ratibiwa pamoja na vijenzi vyake. Machapisho mengi yanayozungumzia hizi nadharia yameandikwa kwa Kiingereza, hivyo basi, ilibidi mtafiti ajitahidi kutafsiri mawazo hayo kwa Kiswahili kinachoweza kueleweka.

Mwisho, mtafiti alikumbwa pia na changamoto ya kutopata muda wa kutosha kutokana na shughuli nyingi anazofanya shuleni anakofundisha. Mahitaji mengi ya shuleni kama vile ufundishaji, utahini na kushiriki katika tamasha za muziki na drama yalifanya mtafiti kutopata muda wa kutosha kushughulikia mambo ya utafiti huu. Kwa hivyo, ilibidi mara kwa mara aahirishe shughuli fulani za utafiti hadi wakati ambapo angepata muda. Licha ya changamoto hizo zote, utafiti huu

haukuathiriwa pakubwa, kwani mtafiti aliweza kukabiliana nazo na hatimaye kukamilisha utafiti huu kwa neema ya Mungu.

## 5.5 Mapendekezo ya utafiti zaidi

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ilidhihirika kwamba zipo changamoto nyingi zinazokumba lugha ya Kiswahili mashinani. Hivyo basi, mtafiti ana mapendekezo yafuatayo ambayo anatarajia kwamba huenda yakawa ya manufaa kwa serikali, wanafunzi, wananchi kwa jumla na pia watafiti wengine ambao wanakusudia kufanya utafiti kuhusu mielekeo ya watu kuhusu lugha ya Kiswahili.

Kwanza, utafiti huu unatoa pendekezo kwa maafisa wanaohusika katika sekta ya upangaji wa lugha na uundaji wa sera za lugha kuweka mikakati inayostahili ili kulainisha matumizi ya lugha nchini Kenya hasa lugha ya taifa. Katika kiwango cha serikali za kaunti, itafaa sana ikiwa wizara ya elimu na ya utamaduni katika serikali ya kaunti ya Nandi itaweka mikakati ya kuajiri wasomi wa kutoa mafunzo ya ziada ya Kiswahili kwa wazawa wa Kinandi ambao wangependa kupata ujuzi zaidi wa Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano yao. Hatua hii itafaa sana hasa kwa wazee waliosoma katika mfumo wa elimu wa zamani (7-4-2-3) ambao haukusisitiza sana mafunzo ya Kiswahili.

Vilevile, tunapendekeza kwamba utafiti wa siku za usoni unaweza kuzingatia sehemu zifuatazo:

Kwa ambavyo uchunguzi huu ulihusu mielekeo ya wauza mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi, tunapendekeza kuwa utafiti kama huu ufanywe kwenye sekta zingine katika kaunti hii ili kubaini mielekeo kuhusu Kiswahili kwenye sekta hizo. Sekta hizo ni kama vile utoaji wa huduma za afya, utumishi wa umma katika wizara za serikali, mashirika ya kibinafsi, vyombo vya habari, asasi za kielimu, na shughuli za kisiasa.

Utafiti huu ulibaini masuala matatu yaliyosababisha mielekeo ambayo ni umri, jinsia na viwango vya elimu. Watafiti wachunguze mambo mengine yanayoweza kusababisha mielekeo kando na yale yaliyoshughulikiwa kwenye utafiti huu. Mambo hayo ni pamoja na mila na desturi, mazingira, sera ya lugha, cheo na shinikizo za marafiki ambao mtu anajihusisha nao.

Utafiti huu uliegemea wafanyabiashara wanaonadi mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi pekee. Utafiti mwingine unaweza kufanywa katika kaunti nyingine tofauti na matokeo yakaweza kulinganishwa ili kuona ikiwa yatafanana ama yatatofautiana na matokeo ya utafiti huu. Itakuwa bora zaidi iwapo utafiti linganishi kama huo utafanywa katika kaunti za wafugaji wa asili ya Kibantu ili kulinganisha mielekeo yao na mielekeo ya wafugaji Wanandi ambayo ni jamii ya asili ya Kinailoti. Kaunti hizo za jamii za Kibantu ni kama vile Busia, Kakamega, na Bungoma ambazo pia huwa na minada ya mifugo.

Mwisho, Baadhi ya wasailiwa katika utafiti huu walidai kwamba hawapendi kutumia Kiswahili kwa ajili ya mawasiliano ya kunadi mifugo kwa madai kwamba ni lugha ngumu. Hivyo basi ipo haja ya watafiti wa baadaye kuchunguza changamoto za kiisimu zinazowakumba Wanandi wanapojifunza Kiswahili Sanifu ili kupendekeza mbinu za kutatua changamoto hizo.

## 5.6 Hitimisho

Kiswahili nchini Kenya kimepewa jukumu la kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi. Wakenya wanapaswa kuienzi lugha hii ya Kiswahili kwa kuwasiliana na wenzao wanapoendesha shughuli zao za kijamii kama kunadi mifugo mnadani.

Kutokana na utafiti huu, imebainika kwamba wauza mifugo mnadani wana mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili. Mielekeo hasi kuhusu Kiswahili imetokana na sababu za kiisimu. Wengi wa wasailiwa walikiri kwamba hawaimudu sarufi ya lugha ya Kiswahili na hivyo basi wanapata changamoto katika kuwasiliana.

Hali ya kupendelea kutumia lugha ya kienyeji iliongozwa na masuala ya kijamii ambapo wauza mifugo walitaka kujihusisha na kuwasiliana na wanajamii moja kwa moja. Hii ilijitokeza wakati mtafiti aliposhiriki utendaji ambapo wafanyabiashara walilalamikia utumiaji wa lugha ya Kiswahili ilhali wanafahamu lugha ya Kinandi.

Umuhimu wa utafiti huu unajitokeza kwa njia mbili: kwanza, utafiti huu utawasaidia washikadau wa masuala ya lugha kubuni mikakati inayohakikisha kwamba wanajamii wote wanafahamu na kutumia Kiswahili kwa ufasaha. Pili, utafiti huu pia utachangia tafiti zilizopo za kurejelewa maktabani kwa lugha ya Kiswahili kuhusu mielekeo ya wauza mifugo mnadani katika kaunti ya Nandi.

# MAREJELEO

Abdullah, N. H., Safrudin, E. M. S. E., Taib, S. A., & Ismail, W. N. F. W. (2018). Language variation according to age: Football talk. *International Journal of Academic Research in Business and Social Sciences, 8*(2), 773–784.

Agheyisi, R., & Fishman, J. (1970). Linguistic attitude studies: A brief survey of methodology approaches, *Anthropological Linguistics* 12 (5), 131-157.

Ajzen, I. (1991). The Theory of planned behaviour. *Organizational Behaviour and Human  Decision Journal*, 50, p179-211.

Ajzen, I., & Fishbein, M. (1980). *Understanding Attitudes and Predicting Social Behaviour*. Englewood. Cliffs, N. J: Prentice Hall.

Ajzen, I & M. Fishbein (2005). The influence of attitudes on behavior. In: Albarracin, D., Johnson, B.T. & Zamnna, M.P. (eds.) *The Handbook of Attitudes. Lawrence Erlbaum Associates.*

Amatubi, M.N. (2002). Globalization and the Mainstreaming of Kiswahili Research in the  21st Century. In: I. Simala (ed). *Utafiti wa Kiswahili* (pp. 43-48). Maseno: Maseno University Press.

Baker, C. (1992). *Attitudes and Language*. Multilingual Matters, Clevedon, UK.

Bhatia, T. K. (2008). *The Handbook of Bilingualism*. (W. C. Ritchie (ed.)). Wiley-Blackwell.

Brown, P. (1980). How and Why are Women More Polite: Some Evidence from a Mayan Community. In M. Ginet, R. Borker, & F. Furman (eds.) *Women and Language in Literature and Society*. Preager Publishers.

Bucker, L. (2018). *Research methods, design and analysis*. SAGE publications.

Bussman, H. (1996). *Routledge Dictionary of Language and Linguistics.* Great Britain: Routledge.

Chaiken, S. & Yates, S. (1985). Affective-cognitive consistency and thought-induced Polarization. *Journal of Personality and Social Psychology*, 49, p.1470-1481.

Chimera, R. (1998). *Kiswahili, Past, Present, and Future Horizons*. Nairobi: Nairobi University Press.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili.* Nairobi: O.U.P.

Coates, J. (2013). *Women, Men and Language: A Sociolinguistic Account of Gender Differences in Language,* 3rd edition. London: Routledge.

Fasold, R. (1984). *The Sociolinguistics of the Society.* London: Basil Blackwell.

Fishbein, M. A. (1967). Attitude and Prediction of Behavior. In M. A. Fishbein (Ed.), *Readings in Attitude theory and measurements* (pp. 477- 492). New York: Willey.

Fishbein, M., & Ajzen, I. (1975). *Belief, Attitude, Intention & Behavior: An Introduction to Theory & Research Reading*. M.A: Addison-Wesley.

Fishbein, M., & Middlestadt, S. E. (1989). Using the Theory of Reasoned Action as a FrameworkFor understanding AIDS-related behavior. In: V. M. Mays, G. W. Albee & S. F. Schneider, (eds.) *Primary Prevention of Aids:Psychological Approaches.* Newbury Park: Sage.

Gardner, R. (1985). *Social Psychology and Second Language Learning: The Role of Attitudes and Motivation*. London: Edward Arnold.

Githinji, P. (2014). Kwa Miaka Hamsini Sheng' Imekitunza Kiswahili au Imekiua? Katika I. Simala, L. Chacha, & M. Osore (wah.) *Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya* (pp. 34-50). Nairobi: Twaweza Communications.

Godin, G., & Kok, G. (1996). The Theory of Planned Behaviour: A Review of its Application to Health- related Behaviours. http://dx.doi.org/10.4278/0890-1171-11.2.87

Gorman, T.P. (1974). The Teaching of Languages at Secondary Level. Katika: W.H. Whitely (mh.) *Language in Kenya.* Nairobi: O.U.P.

Holmes, J. (2013). *An Introduction to Sociolinguistics*. Taylor & Francis.

Iraki, F.K. (2007) Cognitive Efficiency: The sheng Phenomena in Kenya. *International Pragmatics.* Pp. 112-133

Jones, J.M. (2012). The Effect of Language Attitudes on Kenyan takeholder Involvement in Mother Tongue Policy Implementation. *Journal of Multilingual and Multicultural Development,* 33 (3), 237-250.

Kaindi, G.N. (2016). *Mielekeo ya Jamiilugha ya Kimaasai Kuhusu Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Kartz, D.  (1960). "The Functional Approach to the Study of Attitudes." *Public Opinion, 24,* pp. 163-204.

Kibiwott, P.K. (2006). The Future of Languages of Kenya: Adopting the Principles of Environmental Conservation. Makala yaliyowasilishwa katika kongamano la BML Linguistics in Africa, Special Interest Group, Chuo Kikuu cha London.

Kirilenko, S.V. (2024). Language Attitudes: Sociolinguistic aspect. In: *Research Result: Theoretical and Applied Linguistics*, *10* (1) pp. 17-30. DOI: 10.18413/2313-8912-2024-10-1-0-2 https://www.researchgate.net/publications/379907962

Kombo, D. K, & Tromp, D. L. (2006). *Proposal & Thesis Writing*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, C.R. (2004). *Research methodology*. New Delhi: New Age Publishers.

Kotut, L. & McCrickard, D.S. (2022). Winds of Change: Seeking, Preserving, and Retelling Indigenous Knowledge through Self-organized Online Communities. https://dl.acm.org/doi/pdf/10.1145/3491102.3502094 Accessed on 15 Nov. 2025.

Labov, W. (1966). *The Social Stratification of English in New York City.* Washington, D.C: Center for Applied Linguistics.

Lakoff, R. (1975). *Language and women's place.* New York: Harper & Row. https://web.stanford.edu/class/linguist156/Lakoff_1973.pdf

Lezin, N. (2007). Theories and Approaches: Theory of Reasoned Action (TRA). *Resource Center for Adolescent Pregnancy Prevention*. http://www.TRA/TRA- Theories & Approaches

Mackay Report of the Presidential Working Party. (1981). *Second University in Kenya.* Nairobi: Government Printing Press.

Mathooko, P.M. (2007.) *Isimujamii: Misingi ya Nadharia*. Nairobi: Njigua Books.

Mazrui, A.M. (1978). The Religious Factor in Language Nationalism: The Case of Kiswahili in Kenya. Katika *Studies in African Linguistics*, Vol. 9 No. 2, 1978. University of California.

Mazrui, A. M. (1981). *Acceptability in a Planned Standard: The case of Swahili in Kenya*. Unpublished PhD thesis, Stanford University - Stanford.

Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbaabu, I. (1991.) *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Nairobi: Longman Kenya.

Mbaabu, I. (1996). *Language Policy in East Africa: A Dependency Theory Perspective.* Nairobi: Educational Research and Publications.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mesthrie, R., J. Swann, A. Deumert & W.L. Leap. (2000). *Introducing Sociolinguistics.* Edinburgh: Edinburgh University Press, 2000.

Michener, H. A., Delamater, J. D., & Myers, D. J. (2004). *Social Psychology*, Belmont: Thomson-Wadsworth.

Mirianga, R.K. (2014). Mielekeo ya Walimu wa Shule za Msingi kuhusu Suala la Lugha kama linavyoelezwa katika Katiba ya Kenya. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mohochi, E. (2005). *Mielekeo ya Wanafunzi kuhusu Lugha ya Kiswahili na Athari zake katika Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili wa Kidato cha Nne katika Mikoa ya Pwani na Nyanza, Kenya.*Tasnifu ya shahada ya uzamifu isiyochapishwa.Chuo Kikuu cha Egerton - Njoro.

Mohochi, S. (2011).*Mielekeo ya Wasomi wa Kiswahili na Viongozi wa Afrika Mashariki Kuhusu Lugha ya Kiswahili. Swahili Forum. 18:24-36.*

Montano, D. E., & Karsprozy, D. (2002). The Theory of Reasoned Action and Theory of Planned Behaviour. In K. Glanz, B. K. Rimer and F. M. Lewis (Eds.), *Health behavior and Education: Theory, research and Practice* (pp. 67-98) Sanfrancisco: Jossey Bass.

Muaka, L. (2011). Languages Perceptions and Identity among Kenyan Speakers." In: G.B. Eyamba, et.al. (eds.) Selected Proceedings of the 40th Annual Conference on African Linguistics (pp. 217-230). Somerville, MA. Cascadilla Proceedings Project.

Mugenda, O.M. & Mugenda, A.G. (2003). *Research Methods Qualitative and Quantitative Approaches*. Nairobi: Act press.

Mukhwana, A. (2008). *Language Attitude in Urban Kenya: A Case Study of Nairobi, Kisumu and Mombasa*. Tasnifu ya Uzamifu (PhD), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Muthiani, E.N. (1986). *Assesment of possible activities for increased resilience in pastoral communities in Kenya*. Nairobi: Macmillan.

Muthwii, M.J. (2002). *Language Policy and Practices in Education in Kenya and Uganda: Perception of Parents, Pupils and Teachers on the use of Mother Tongue, Kiswahili and English in primary schools*. Nairobi: Phoenix.

Mwaro, A.G. (2002). Mchango wa A.S. Nabhany katika Utafiti na Utandaridhi wa Istilahi za Kiswahili. Katika: I. Simala (ed). *Utafiti wa Kiswahili (*uk. 49 – 56). Maseno: Maseno University Press,.

Myers-Scotton, C. (1997). Functions of Code-Selection. In: R.K. Herbert (ed.) *Language and Society in Africa: The Theory and Practice of Sociolinguistics,* (pp. 165–80). Johannesburg: Witwatersrand University Press.

Njoroge, D. (1990). *Kikuyu Deverbative and other Nominations*. M.A Thesis, University of Nairobi. (Unpublished)

Nyandwaro, K.L. (2015). *Mielekeo ya Wafanyakazi kuhusu Kiswahili kama Lugha Rasmi katika Wizara za Serikali nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili isiyochapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Ogola, J. O. (1990). *Mielekeo ya Wasomi kuhusu Matumizi ya Lugha ya Kiswahili nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili isiyochapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Ohia, B.F. (2023). Linguistic Features of Code-Mixing and Code-Switching: The Case of Educated Ogba Bilinguals. *European Journal of Theoretical and Applied Sciences, 1*(3), 392-399.

Ominde, H. S (1964). *Report on reforms of Kenya's Education system*. Nairobi: Oxford University Press.

Oppenheim, A.N. (1966). *Questionnaire Design and Attitude Measurement*. London: Heinemann.

Owalo, A. (2014). *Mitazamo kuhusu Kiswahili Miongoni mwa Wazungumzaji wa Kiluo: Kifani cha Shule za Msingi katika Kaunti ya Migori:* Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu Nairobi.

Republic of Kenya. (2010). *The New Constitution of Kenya.* Nairobi: Government Press.

Ringle, A. (2024). The difference between male and female brains. https://www.endeavorhealth.org/articles/differences-in-men-women-brains Retrieved on 3-11-2025.

Ritchie, J. na Lewis, J. (2003). *Qualitative Research Practice: A Guide for Social Sciences Students and Researchers.* London: Sage Publications.

Ryanga, C.S.W.A. (2001). Reaching out for Linguistic Identity: The State of Kiswahili in Kenya. In: N.I. Shitemi, M.N. Noordin, A.I. Opijah & D.M. Mukuriah (eds.) *Kiswahili: A Tool for Development – The Multidisciplinary Approach* (pp.24 – 35). Eldoret: Moi University Press.

Shazu, R. I. (2014). Relationship between Gender and Language. In: *Journal of Education and Practice*. Vol. 5, No. 14. pp. 93-100. www.iiste.org

Smith,R.G. (1996). *The history of the term 'Secular'*. Collins Clear Types Press, London, 141.

Thiong`o, N. (1986). *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Tlou, E.R. (2009). *The Application of the Theories of Reasoned Action and Planned Behaviour to a Working Place HIV/Aids Health Promotion Programme.* Unpublished PhD Thesis, University of South Africa. http://r.sear.urRc6zvgVVM.

Triandis, H.C. (1971). *Attitude and Attitude Change.* Illinois. John Wiley and Sons, Inc.

Trudgill, P. (1983). *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society,* 2nd edition. Harmondsworth: Penguin.

Tsunoda, T. (2006). *Language Endangerment and Language Revitalization: An Introduction*. German: Mounton De Gruyter.

Webb, V. & Kembo-Sure (wah) (2000). *African Voices: An Introduction to Language and Linguistics of Africa.* Southern Africa: Oxford University Press.

Wendo, N. (2009). Language policy in Kenya: Negotiation with Hegemony. *The Journal of Pan African Studies*, Vol. 3 No.1 pp. 121-138.

Whiteley, W.H. (1969). *Swahili: The Rise of a National Language*. London: Methuen.

***

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1

### Barua ya kujitambulisha kwa wasailiwa

ANNE JEPKEMBOI,

S.L.P 135,

Songhor

2021

Kwa Bw./ Bi. ________________________________

**KUH : MIELEKEO YA WAUZA MIFUGO MNADANI KUHUSU KISWAHILI KATIKA KAUNTI YA NANDI**

Mimi ni mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ninafanya utafiti kuhusu mada iliyotajwa hapo juu. Naomba unisaidie kujaza Hojaji zilizoambatanishwa na barua hii kwa uaminifu. Nakuahidi ya kwamba majibu yako pamoja na utambulisho wako vitakuwa vya siri kabisa. Habari nitakazozipokea kutoka kwa Hojaji zenyewe zitatumiwa tu katika utafiti wangu. Asante kwa ushirikiano wako.

Wako Mwaminifu,

*AJepkemboi*

Anne Jepkemboi

## Kiambatisho 2

### Hojaji kwa wauza mifugo minadani

Kwa msailiwa mpendwa,

Naomba uitikaji wako kuhusu maswali nitakayouliza. Huu ni utafiti wa kiakademia kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa wauza mifugo mnadani katika kaunti ndogo ya Nandi. Habari nitakazopokea kutoka kwa hojaji zitakuwa za siri kabisa.

Usiliandike jina lako popote.

1. Taja jinsia yako (Tia alama(√) ) Mke ☐ Mume ☐

2. Tia alama (√ ) kwenye umri wako.

   Chini ya miaka 20-30 ☐

   Kati ya miaka 31-40 ☐

   Kati ya miaka 41-50 ☐

   Zaidi ya miaka 51 ☐

3. Tia alama ( √ ) kwenye kiwango chako cha elimu.

   Shule ya Msingi ☐

   Shule ya Upili ☐

   Chuo anuai ☐

   Chuo kikuu ☐

4. Unaweza kuzungumza lugha zipi? Tia alama (√)

   Kiswahili ☐ Kiingereza ☐ Kinandi ☐ Kuchanganya zote ☐

5. a) Unapendelea kutumia lugha ipi unapofanya biashara ya kuuza mifugo mnadani? Kinandi ☐ Kiswahili ☐ Kiingereza ☐ Kuchanganya yote ☐ b) Toa sababu zinazokufanya wewe kupendelea lugha hiyo.

6. a) Kwa maoni yako kuna manufaa ya lugha ya Kinandi kutumika katika biashara ya kuuza mifugo mnadani? Ndio ☐ La ☐

   b) Eleza sababu za jibu lako.

7. a) Je, una maoni gani kuhusu Katiba ya Kenya kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa nchini?

   b) Je, kuna manufaa gani kwa Kiswahili kutumika katika biashara ya kuuza mifugo mnadani?

8. Taja changamoto za kiuelewa ambazo unakumbana nazo unapowasiliana na wateja wako mnadani unapotumia lugha ya Kiswahili.

9. Je, unaweza kusemaje kuhusu upeo wako wa matumizi ya lugha zifuatazo? (Chagua mojawapo ya majibu haya kwa kila lugha: Upeo wa juu, upeo wa kati, upeo wa chini) .

   a)Kiswahili ☐

   b)Kinandi ☐

   c)Kiingereza ☐

10. a) Ni lugha ipi unayofikiria inakuwezesha kuwasiliana na wateja wako vizuri? Kiswahili ☐ Kinandi ☐ Kiingereza ☐

    b)Toa sababu

11. Kwa ujumla kama mfanyabiashara una mielekeo gani kuhusu lugha ya Kiswahili? Ninakipenda ☐ sikipendi ☐ Chagua kwa kuweka alama (√)

Nashukuru sana kwa muda ulionipa. Mchango wako umekuwa muhimu sana katika utafiti huu.

## Kiambatisho 3

## Maswali ya viwango kwa wauza mifugo mnadani

Tafadhali weka alama ya mviringo (0) kwenye kauli ulizopewa hapo chini ukionyesha kwamba;

Nakubaliana kabisa (1)

Nakubaliana (2)

Nakataa (3)

Nakataa kabisa (4)

1. Naipenda lugha ya Kiswahili.

1 2 3 4

2. Lugha ya Kiswahili ina manufaa katika maisha kwa jumla.

1 2 3 4

3. Naridhishwa na nafasi ya Kiswahili nchini.

1 2 3 4

4. Lugha ya Kiswahili hutumika katika shughuli mbalimbali za kijamii wakati wowote.

1 2 3 4

5. Kiswahili ni kigumu mno.

1 2 3 4

6. Natumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na wenzangu mnadani.

1 2 3 4

7. Lugha ya Kiswahili ina manufaa kwangu kama Mkenya.

1 2 3 4

8. Siridhishwi na jinsi Kiswahili kilivyofunzwa shuleni.

1 2 3 4

9. Lugha ya Kiswahili ni lugha inayostahili kutumika katika mawasiliano yetu ya kila siku.

1 2 3 4

10. Ujuzi wa lugha hii ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa hutegemea mazingira alimokulia mzungumzaji.

1 2 3 4

## Kiambatisho 4

## Bajeti ya pendekezo

| **MAELEZO** | **GHARAMA** |
|---|---|
| 1. UCHAPISHAJI WA KAZI<br>Kununua tarakilishi<br>Kuchapisha pendekezo | <br>50, 000<br>5,000 |
| 2. VIFAA VYA KUANDIKIA<br>Vifaa vya kuandikia<br>Karatasi za kurudufia<br>Kalamu, vifutio, penseli | <br>1,000<br>1,500<br>200 |
| 3. USAFIRI<br>Kupeana Hojaji<br>Kushauriana na wasimamizi | <br>1,000<br>30,000 |
| 4. KUUNGANISHA TASNIFU<br>Kuunganisha pendekezo | <br>1,000 |
| 5. ANUWAI | 15,000 |
| **JUMLA** | **104,700** |

## Kiambatisho 5

## Kibali cha utafiti

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **253993** Date of Issue: **30/March/2021**

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Ms.. Jepkemboi Anne of Kenyatta University, has been licensed to conduct research in Nandi on the topic: Mieleko ya wauza mifugo mnadani kuhusu kiswahili katika kaunti ya Nandi for the period ending : 30/March/2022.**

License No: **NACOSTI/P/21/9759**

**253993**
Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013

The Grant of Research Licenses is Guided by the Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

CONDITIONS

1. The License is valid for the proposed research, location and specified period
2. The License any rights thereunder are non-transferable
3. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research
4. Excavation, filming and collection of specimens are subject to further necessary clearence from relevant Government Agencies
5. The License does not give authority to tranfer research materials
6. NACOSTI may monitor and evaluate the licensed research project
7. The Licensee shall submit one hard copy and upload a soft copy of their final report (thesis) within one year of completion of the research
8. NACOSTI reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice

National Commission for Science, Technology and Innovation
off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623, 00100 Nairobi, KENYA
Land line: 020 4007000, 020 2241349, 020 3310571, 020 8001077
Mobile: 0713 788 787 / 0735 404 245
E-mail: dg@nacosti.go.ke / registry@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke

**Kiambatisho 6**

**Ramani ya Kaunti ya Nandi**




Chanzo: https://regreeningafrica.org